




UKURASA 3

**MBUNGE** aingia hofu ubadhirifu wa milioni 300/ -


Wataka ada kuchaacha, kuache rdugo
BUFE
JUMA, MACHI 4, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA
SIDO ilivyowainua wajasiriamali Morogoro kupitia kongano bidhaa
KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI
Shujaa aliyetumikia jiko kuu Ikulu, sasa anawanoa wa shahada upishi
- Aanika kujiamini kulivyompa majibu
- Msimamo wake umebaki kuwa nguzo

# Nipashe

Ijumaa Machi 4, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • No. [illegible]0874

MWANGA WA JAMII

www.ippmedia.com
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

UKURASA 11

# KUMEKUCHA




CAG Charles Kichere

**CAG** aanza kukagua fedha za UVIKO- 19, 'wapigaji' kukalia kuti kavu... *Endelea ukurasa 2*

# Pinda ataja dawa kukomesha mauaji

UKURASA 2



UKURASA WA 4

## MBOWE KUANZA KUJITETEA LEO

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake

UKURASA WA 4

## MWINYI AITWISHA MZIGO TCB KUINUA WANAWAKE KIUCHUMI

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa serikali anayoiongoza lengo lake ni kuubadilisha uchumi wa Zanzibar...

## Mhadhiri chuo asimamishwa kwa tuhuma za rushwa ngono

UKURASA 3



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, akimsikiliza Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Biashara Tanzania (TCB), Sabasaba Moshingi (wapili kushoto), alipofika na ujumbe wake Ikulu, jijini Zanzibar jana, kwa ajili ya mazungumzo na kujitambulisha. Kushoto ni Mkurugenzi wa Sheria wa benki hiyo, Mystca Mapunda Ngongi. **Habari Uk. 4. PICHA: IKULU**

**MICHEZO** **SIMBA, BIASHARA KUMALIZA UBISHI** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Kumekucha fedha za UVIKO-19

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KUMEKUCHA! Ndivyo unavyoweza kusema baada ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kutangaza kuwa ameanza kufanya ukaguzi maalumu wa matumizi ya fedha za UVIKO-19 zilizopelekwa kwenye halmashauri nchini.

Vilevile, Katibu Mkuu Kiongozi, Balozi Hussein Katanga, amekubali kushughulikia ombi la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kupatiwa watumishi 104 ili kuondokana na kuchelewa kwa ukaguzi kwenye maeneo mbalimbali nchini.

CAG, Charles Kichere, alibainisha kuanza kwa ukaguzi huo maalumu jana wakati wa kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi hiyo kilichofanyika jijini hapa.

"Tunampongeza Mheshimiwa Rais Samia kwa namna anavyokabiliana na janga la UVIKO-19. Ninampongeza Rais kwa namna alivyotoa maelekezo ya matumizi ya fedha za kukabiliana na UVIKO-19, hususan afya, elimu, maji na hatua anazochukua za kudhibiti matumizi ya fedha hizo,"alisema.

Alibainisha kuwa katika kuunga mkono jitihada hizo, ofisi yake imeanza kutekeleza jukumu lake la katiba kwa kuanza ukaguzi kwenye halmashauri zilizopata fedha hizo.

"Mheshimiwa mgeni rasmi (Katibu Mkuu Kiongozi) nikuhakikishie kwamba tutafanya ukaguzi wa fedha hizo zote za UVIKO-19 zilizoletwa na kila senti ya fedha hizo itakaguliwa na taarifa itatolewa, ili kuhakikisha fedha hizo zimetumika kulingana na maelekezo, taratibu, sheria na miongozo ya matumizi ya fedha za umma," alisema.

Akifungua kikao hicho, Balozi Katanga alikubali ombi la ofisi hiyo kupatiwa watumishi 104 ili kukabiliana na upungufu uliopo unaosababisha baadhi ya shughuli za ukaguzi kuchelewa. Alisema lengo kubwa ni kuiwezesha ofisi hiyo kufanya kazi kwa weledi huku akiwaasa kujiepusha na vitendo vya utovu wa nidhamu, ikiwamo kupokea rushwa wakati wanatekeleza majukumu yao.

"Ni dhamira ya serikali kuhakikisha fedha zinazopelekwa kwenye miradi ya maendeleo zinatumika vizuri na thamani ya fedha inapatikana," alisema. Balozi Katanga alisema kuwa katika kupunguza hoja za ukaguzi kwenye wizara na taasisi za umma, ni vyema ofisi yake na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali washirikiane ili kuhakikisha kunakuwa na uwazi na uwajibikaji kwenye mapato na matumizi ya rasilimali nchini.

"Ofisi hii inapaswa kufanya kazi kwa uhuru bila kuingiliwa na mtu yeyote. Niwapongeze sana watendaji kwa kutoa ripoti na kutekeleza majukumu ya ukaguzi maalum ambao huombwa na viongozi au taasisi," alisema.

Awali, Mkurugenzi Msaidizi wa Rasilimali Watu na Utawala wa Ofisi hiyo, Godfrey Mgomi, alisema lengo ni kujadili na kujibu hoja za watumishi kupitia mpango mkakati wa ofisi hiyo, kupitia maoteo ya bajeti na kupata tathmini ya utekelezaji wa bajeti inayoisha 2021/22.

Mwaka jana, Tanzania ilipatiwa mkopo wa dharura wa Sh. trilioni 1.29 na Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) kwa ajili ya kukabiliana na athari za ugonjwa wa UVIKO-19. Kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 230 zilipelekwa Tanzania Zanzibar.

Baada ya kuripotiwa kuwapo hofu ya 'upigaji' wa fedha hizo katika baadhi ya halmashauri, serikali iliagiza kufanyike ukaguzi maalumu kuhusu matumizi ya fedha hizo, huku Rais Samia Suluhu Hassan akionya kuwa yeyote atakayebainika kufuja fedha hizo 'ataijua sura yake halisi'.

# Pinda ataja dawa kukomesha mauaji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WAZIRI Mkuu mstaafu, Mizengo Pinda, amesema dawa pekee ya kukomesha mauaji nchini ni kushirikisha viongozi wa dini ili kuhubiri na kuelimisha jamii kuachana na matukio hayo.

Pinda ambaye ni mlezi na mwanzilishi wa Jumuiya ya Maridhiano Tanzania, aliyasema hayo jana kwenye maadhimisho ya Siku ya Maridhiano iliyofanyika jijini hapa. Mgeni rasmi alikuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema kitu kilichosaidia kukabiliana na mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi mwaka 2008 wakati akiwa Waziri Mkuu serikali iliwashirikisha viongozi wa dini na kufanikiwa kupunguza mauaji hayo.

"Mwaka 2008 nilionja joto ya jiwe mauaji ya Watanzania wenzetu wenye ualbino. Haikuwa kazi ndogo na halikuwa jambo jema. Serikali tulijitahidi kwa kutumia vyombo vyetu kamata huyu, lakini ilikuwa kama vile unachochea, ikafika mahali nikasema hapana lazima tutafute njia nyingine. Hiyo ndiyo sababu ya kuanza kushirikisha viongozi wa dini wote baada ya kutambua kwamba mauaji haya mengine ni ujinga tu, yanatokana na ushirikina.

"Hawa watu hawajaguswa na neno la Mungu, hivyo hawana hofu na Mungu. Dawa ni hawa viongozi, sisi kauli za kiserikali na maeneo ya kisiasa ilikuwa ngumu. Tuliomba sana viongozi hawa tukae pamoja kuelimisha jamii kukomesha mauaji hayo. Tulipokewa vizuri na kuanza kufanya kazi hasa Kanda ya Ziwa ambako mauaji yalikuwa mengi, nikaona mambo kidogo yananza kubadilika... lakini kwa sasa ni kuwaasa watu waache mauaji na hata mauaji ya Kiteto niliyakomesha," alisema.

Alibainisha kuwa hali hiyo ilimjenga na alikuwa akifanya vikao na hatimaye kufanikiwa kupunguza mauaji na hivyo kuja na wazo la kuanzisha jumuiya hiyo mwaka 2014.

**KAULI YA WAZIRI**

Naye Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni, alisema taifa lina wajibu wa kushirikiana kutatua kero hiyo.

"Katika kipindi cha hivi karibuni tarehe za kwanza za Januari hadi Februari mwanzoni, tumeshuhudia matukio ya mauaji nchini na ukifuatilia sababu zake zinakuwa ambazo zinashangaza na za aibu. Kwa mfano, wako watu wanachukua sheria mkononi kwa sababu wanagombea mali na ni ndugu wa familia moja. Wengine wanafanya haya matendo kwa sababu ya ramli chonganishi," alisema.

Masauni alisema kuna watu wanajifanya waganga wanashiriki kuwapa taarifa za uongo na kuhamasisha kuchochea mauaji kwa jamii huku akibainisha kuwa chanzo kingine ni wivu wa mapenzi na wivu wa kupindukia jambo ambalo halikubaliki kwa jamii.

"Kwa siku za hivi karibuni yameonekana kupungua kama ambavyo amezungumza mlezi (Pinda). Kama watu hawa wangekuwa na hofu ya Mungu, wasingefanya haya. Hakuna kitabu cha dini kinachokubali matukio ya mauaji. Hii niache kama changamoto kwenu kwamba mna wajibu wa kuhakikisha tunaondokana na hali hiyo," alisisitiza.

**SPIKA MAKINDA**

Mjumbe wa Kamati ya Maadili wa Jumuiya hiyo, Spika mstaafu Anne Makinda, alisema matukio ya mauaji yanayotokea kwa sasa watu wameondoa utu kwenye akili na mioyo ya watu na kutaka kurudi kwenye mila na desturi ili kuacha kuuana.

"Neno kuua hakikuwa kitu rahisi kusema. Kuona maiti tu mtoto alikuwa haruhusiwi kuona. Haya maneno tunayosema hapa tunaweza tusieleweke, kila mtu achukue kwenye moyo wake afikirie angekuwa katika nchi zile zinazopigana sasa yeye akawa raia pale. Inawezekana fujo za mtu mmoja mmoja zikaleta vitendo vya kulipizana kisasi. Mtu anabeba mambo yake moyoni mpaka atimize nyie hamfahamu," alisema.

"Mauaji yaliyotokea Bahi juzi yalikuwa kweli ni lazima? Kwa hiyo ndugu zangu tumshukuru Mungu kwa haya na viongozi wetu wa maridhiano. Kitu kidogo kinaweza kuvuruga amani ya nchi yetu kila mmoja ahakikishe anakuwa mlinzi wa mwenzake," alisema.

**MWENYEKITI MARIDHIANO**

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo na Shekhe wa Mkoa wa Dar es Salaam, Alhad Mussa Salum, alisema jumuiya hiyo inalaani mauaji yanayotokea na kuahidi kuendelea kushirikiana na serikali ili kukomesha mauaji.

Alimpongeza Rais Samia kwa kuimarisha uchumi, siasa na demokrasia huku akiahidi viongozi hao wataitunza jumuiya hiyo kwa maslahi mapana ya taifa.

## Viongozi wa dini washtuka wahitimu vyuo kutokujiajiri

**Na Mwandishi Maalum**

RAS Samia Suluhu Hassan amekutana na viongozi wa dini mbalimbali na kujadili masuala ya maendeleo ya nchi katika kikao kilichofanyika Ikulu jijini Dar es Salaam juzi.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari juzi usiku na Mkurugenzi wa Mawasiliano Ofisi ya Rais, Ikulu, Zuhura Yunus, miongoni mwa masuala waliozungumzia ni elimu.

Alibainisha kuwa katika hilo viongozi hao wamependekeza kuwapo na mjadala mpana kuhusu mfumo mpya utakaokidhi mahitaji ya sasa kwa maana ya kutozalisha jamii ya wahitimu walioandaliwa kuajiriwa peke yake.

Rais Samia katika mkutano wake na vijana jijini Mwanza mwaka jana, alibainisha kuwa Tanzania kuna jumla ya vijana milioni 20.7 wenye umri kati ya miaka 15 na 35, lakini ndani ya kundi hilo, asilimia 11.4 ya wenye sifa za kuajiriwa, hawako kazini.

Vilevile, taarifa ya Ikulu ilibainisha kuwa viongozi wa dini wameomba kutotozwa kodi ya mapato kwenye fedha ambazo zinapatikana kama misaada ya hiari ya wanachama na wafadhili kwa ajili ya kuendesha huduma zisizo za kibiashara, zikiwamo huduma za wajane na yatima.



Makamu wa Rais, Dk. Philip Mpango, akisalimiana na Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, kabla ya mazungumzo yao yaliyofanyika ukumbi wa mikutano wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Mazingira (UNEP), jijini Nairobi, Kenya jana. **PICHA: OMR**

HABARI KITAIFA

# Mhadhiri asimamishwa kazi tuhuma za rushwa ya ngono

**Na Daniel Sabuni,** ARUSHA

TUHUMA kuhusu picha chafu za rushwa ya ngono zinazosambaa mitandaoni zikidaiwa kumhusisha Mhadhiri wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA), Adam Semlambo, zimesababisha menejimenti ya chuo hicho kumsimamisha kazi ili kupisha uchunguzi.

Uamuzi wa kumsimamisha kazi mhadhiri huyo ulitolewa juzi na Kaimu Mkuu wa Chuo hicho, Dk. Cairo Mwaitete, kupitia tangazo lake la taarifa kwa umma kuhusiana tuhuma hizo.

Katika barua yake, Dk. Mwaitete alisema uongozi wa Chuo cha Uhasibu Arusha umepokea kwa masikitiko taarifa iliyosambaa katika mitandao ya kijamii ikimwonyesha mmoja wa wafanyakazi wa IAA, Adam Semlambo, mwenye cheo cha mhadhiri, ikimtuhumu kuhusika na picha chafu zinazosambaa kwenye mitandao.

"Chuo cha Uhasibu Arusha kama taasisi ya umma, kinapinga vitendo vyote vibaya visivyoendana na maadili ya utumishi wa umma.

"Hivyo, ili kupisha uchunguzi wa tuhuma hizo, mhadhiri huyo amesimamishwa kazi kuanzia leo tarehe 2/3/2022 mpaka hapo uchunguzi utakapokamilika kwa mujibu wa taratibu za kisheria," Dk. Mwaitete alibainisha katika taarifa yake hiyo.

Dk. Mwaitete alisema IAA pia inafanya mawasiliano na vyombo vinavyohusika na uchunguzi kwa hatua zaidi na kwamba wao kama chuo wanaahidi kutoa ushirikiano kwa vyombo husika.

Ili kuthibitisha ukweli wa barua hiyo, Nipashe iliwasiliana na Ofisa Uhusiano wa Chuo cha Uhasibu Arusha, Sarah Goroi, ambaye alikiri kuwa barua hiyo ya chuo hicho na tuhuma ni hizo wanazifanyia kazi. "Taarifa hiyo ni ya kwetu, kuna tuhuma hizo na zimeshawasilishwa tayari kwa mamlaka husika kwa ajili ya uchunguzi," alisema Goroi. Alipotafutwa kuzungumzia tuhuma hizo, Mkuu wa Taasisi Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Arusha, James Ruge, alijibu kwa kifupi, akisema: "Hata kama tunafanya uchunguzi, tutoe kwenye vyombo vya habari? Mzee (mwandishi), kazi inafanyika. Asante!" Ni sura ya kashfa inayojitokeza huku kukiwapo historia ya tuhuma zinazofanana na hizo katika taasisi za elimu ya juu nchini, ikijumuisha vyuo vikuu kadhaa na taasisi ya elimu ya juu zinazomilikiwa na serikali, pia kadhaa binafsi.

Desemba 27, 28 na 29 mwaka 2019, Nipashe ilichapisha ripoti maalumu kuhusu kashfa ya rushwa ya ngono vyuo vikuu, ikihusisha: Mhadhiri kwa mwanafunzi; mwanafunzi kwa mwanafunzi; mhadhiri kwa mhadhiri; na mhadhiri/ofisa utawala na mfanyakazi wa ngazi ya chini chuoni.

Katika ripoti hiyo, TAKUKURU ilibainisha kuwa asilimia 18 ya wanafunzi wa elimu ya juu na kinamama wajasiriamali wanatumikishwa kwa rushwa ya ngono nchini.

Vilevile, mwaka 2016, serikali katika kukabiliana na aina hiyo ya rushwa, ilifanya marekebisho ya Sheria ya Uhujumu Uchumi ya Mwaka 1984 na marejeo yake ya mwaka 2002 na kuifanya rushwa ya ngono kuangukia kwenye jinai ya Uhujumu Uchumi. Adhabu yake ni kifungo cha hadi miaka 20 gerezani.



Mchungaji wa Kanisa la Mfalme Zumaridi, Diana Bundala, akishuka katika gari la polisi, baada ya kufikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi wa Mkoa wa Mwanza jana, kwa ajili ya kusomewa mashtaka matatu likiwemo la usafirishaji haramu wa binadamu yanayowakabili yeye na wenzake 92. **PICHA: ROSE JACOB**

# Mbunge ahofia ubadhirifu mil. 300/-

**Na Hamida Kamchalla,** KOROGWE

MBUNGE wa Korogwe Vijijini, Timotheo Mnzava (CCM), amedai kuingiwa na hofu ya matumizi mabaya ya fedha za umma na kusuasua kwa kasi ya ukusanyaji wa mapato katika Wilaya ya Korogwe mkoani Tanga.

Amesema hofu hiyo inatokana na kile anachodai halmashauri inajiendesha bila kufuata kanuni katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha ndani.

Mbunge aliibua hofu hiyo juzi wakati wa kikao cha kawaida cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri hiyo.

"Ninaona kuna viashiria vya ubadhirifu vinavyoendelea, baadhi ya watendaji wa halmashauri hawatii maagizo ya Baraza la Madiwani.

"Sasa, kama baraza litashindwa kuchukua hatua kurekebisha hali hii, nitachukua uamuzi mgumu wa kutoa taarifa kwa Chama Cha Mapinduzi (CCM), lakini pia TAMISEMI (Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa).

"Halmashauri hii ni mojawapo ya halmashauri ambazo zinakwenda ovyo, na siko tayari kuwa sehemu ya hayo. Nitahakikisha ninasimamia ukweli, hata kama itanigharimu kuachia ngazi, niko tayari," alisema.

Mbunge huyo aliyataja baadhi ya mambo anayoyaona yanakwenda isivyo kuwa ni ubadilishaji wa matumizi ya fedha bila kuzingatia kanuni.

"Kuna fedha takribani Sh. milioni 300, ambazo zilikusanywa na kutumika bila kufikishwa benki na kuna Sh. milioni 18, ambazo zilitolewa katika fungu la Sh. milioni 240 zilitolewa kwa ajili ya mpango wa Kupanga,

Kupima na Kukamilisha Ardhi (KKK) bila kufuata kanuni.

"Fedha zile zilitolewa kuwapa makundi maalumu - kinamama na vijana ambao walipaswa kupewa fedha kutokana na mikopo ya ndani. Uzembe umesababisha fedha zisipatikane kwa wakati kuendeleza miradi ile muhimu kwa wananchi," alilalamika.

Akizungumzia hoja ya mbunge huyo, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Sadiki Kalaghe, alisema tayari baraza lake, limemwagiza Mkurugenzi Mtendaji na menejimenti yake kupeleka kwenye baraza taarifa ya mapato na matumizi ya kuanzia mwezi Julai hadi Desemba mwaka jana, baada ya kutoridhika na utendaji wao.

"Menejimenti tumeipa wiki mbili kupeleka taarifa ya miradi ya jengo la utawala la halmashauri hiyo, wodi tatu za Hospitali mpya ya Wilaya, ukamilishaji wa zahanati tatu pamoja na ujenzi wa vituo vya afya vitatu vya kata za Mnyuzi, Kerenge na Miumbara.

"Vilevile, kikao hiki cha Baraza la Madiwani kinatoa siku tatu kwa menejimenti kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Mabasi Mombo, ambao umekuwa ukisuasua kwa muda mrefu sasa," alisema.

Akizungumzia madai hayo ya udhaifu wa kiutendaji, Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, Basila Mwanukuzi, alisema: "Kama hatukusimamia utendaji lawama zote zitaturudia sisi na kama tulishiriki, pia lawama bado zitaturudia, ni lazima tufanye mambo kwa umakini mkubwa. Uongozi ni dhamana kubwa sana katika kuhakikisha mambo yanakwenda sawa."

Alipotafutwa kwa njia ya simu kuzungumzia madai hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, Halfan Magani, alitoa ufafanuzi kuhusu hoja ya mbunge huyo.

Magani alisema madai kwamba Sh. milioni 300, fedha mbichi, zimeliwa si ya kweli kwa kuwa anachokifahamu ni Sh. milioni tatu ambazo zilikusanywa na mtendaji wa kijiji katika Kata ya Mmbale ambaye kwa sasa ni marehemu na fedha zipo katika ofisi ya mweka hazina.

"Tulimpa mashine ya posi kwa ajili ya kukusanya mapato lakini katikati akaanza kuumwa na kumkabidhi mwenzake mashine ili aendelee kukusanya mapato.

"Aliugua muda mrefu takribani miezi mitatu. Kwa hiyo, alitumia kama Sh. milioni moja na kidogo kujiuguza kabla hajaingiza kwenye mfumo na baadaye alifariki.

"Yule mtendaji aliyeachiwa kukusanya, aliendelea. Akafikisha Sh. milioni tatu na kidogo akaileta kwetu tukaipokea. Sasa posi mashine haikubali kuingiza fedha nusu," alisema.

Magani aliendelea kufafanua: "Kwa hiyo, sisi hatukuweza kujiingizia, hivyo tumeandika barua TAMISEMI kuwasilisha kifo cha mtendaji ambaye amefariki dunia na iwafutie deni lile na kuingiza zile fedha.

"Bado hawajatujibu na huwa wanajibu kwa kuruhusu mfumo kufanya kazi, wakiruhusu tutaingiza, hiyo fedha mbichi inayosemwa ndiyo hiyo Sh. milioni tatu ambayo tunayo na siyo Sh. milioni 300."

Pia alifafanua kuhusu Sh. milioni 18 za mradi wa KKK, akisema fedha za mradi huo zimechanganywa kwenye akaunti na za miradi mingine zinaingizwa huko, hivyo fedha zilizotolewa siyo za mradi bali ni za halmashauri ambazo hutolewa asilimia 10 kwa makundi maalumu.

"Zile fedha ni kwamba sisi tunavyokusanya tunatakiwa kupeleka asilimia 10 kwenye vikundi vya kinamama, vijana na watu wenye ulemavu.

"Sasa fedha ilitoka kwenye akaunti ya pamoja ambayo inapokea fedha za aina tofauti tofauti, hizo fedha za mradi wa KKK zimo humo, kuna fedha za miradi mingine, lakini kuna fedha za halmashauri zimo humo.

"Kwa hiyo, sijajua wamechukua kigezo gani cha kusema kwamba fedha hiyo imetoka kwenye mradi wa KKK, lakini kwenye hiyo akaunti kuna fedha zaidi ya Sh. milioni 700, halafu sasa kingine ni kwamba tumetoa hiyo fedha hatukuitumia kwa matumizi tofauti tumeipeleka kwenye ile asilimia 10 ya makundi maalumu."

Kuhusu kumalizika kwa miradi ya maendeleo ikiwamo hospitali ya wilaya, vituo vya afya vitatu, zahanati tatu, jengo la utawala pamoja na stendi ya mabasi ya Mombo, mkurugenzi huyo alisema fedha alizopokea, zikiwamo za mradi wa Kituo cha Afya Mnyuzi, ziliingia Novemba mwaka jana na miradi mingine yote alikuta imeshaanza kutekelezwa.

"Hii miradi yote ambayo imeongelewa sasa hivi, ukiachana na mradi wa Kituo cha Afya Mnyuzi, tumepokea fedha mwezi wa 11 mwaka jana, na tumeanza kutekeleza wakati mimi nipo, lakini inayobaki yote wakati nakuja kukabidhiwa kituo cha kazi nikakuta imeshatekelezwa na fedha zimeisha," alisema.

# Mbowe kuanza kujitetea leo

Na Kulwa Mzee

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe na wenzake watatu wanaokabiliwa na mashtaka ya ugaidi, wanatarajiwa kuanza utetezi leo.

Washtakiwa hao watatoa ushahidi wa utetezi Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi mbele ya Jaji Joackim Tiganga mkoani Dar es Salaam.

Mahakama ilifikia hatua hiyo baada ya kuwaona washtakiwa wana kesi ya kujibu katika uamuzi wake wa Februari 18, mwaka huu.

Washtakiwa walionekana wana kesi ya kujibu katika mashtaka matano huku shtaka la sita lililokuwa linamkabili mshtakiwa wa kwanza, Halfani Bwire, la kukutwa na vifaa mbalimbali vya jeshi, zikiwamo sare, likiondolewa.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, Bwire, Adamu Kasekwa, maarufu Adamoo, na Mohammed Ling'wenya.

Wakili wa mshtakiwa wa kwanza Bwire, Jeremiah Mtobesya alidai mteja wake atajitetea mwenyewe chini ya kiapo na anategemea kuita mashanidi wengine watano na yeye atakuwa wa sita na vielelezo vitano.

Wakili John Mallya kwa niaba ya mshtakiwa wa pili, Kasekwa, alidai wanatarajia kuleta mashahidi watatu pamoja na Kasekwa, hivyo watakuwa wanne na vielelezo vinne.

Wakili wa mshtakiwa wa tatu, Mohammed Ling'wenya, Fredrick Kihwelo, alidai mteja wake atajitetea kwa kiapo na atakuwa na mashahidi sita na vielelezo sita.

Wakili Peter Kibatala alidai Mbowe atajitetea chini ya kiapo na atakuwa na mashahidi 10 na yeye mwenyewe na vielelezo 20.

Washtakiwa wanatuhumiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi kati ya Mei na Agosti 5, 2020 maeneo ya Moshi, Arusha, Mbeya, Morogoro na Mwanza.

Katika shtaka la kwanza, washtakiwa wote wanadaiwa kati ya Mei Mosi na Agosti 5, 2020, maeneo ya Hoteli ya Aishi, Kilimanjaro walikula njama ya kutenda vitendo vya ugaidi, kulipua vituo vya mafuta na mikusanyiko ya watu kwa lengo la kuleta hofu kwa Watanzania.

Kwenye shtaka la pili, inadaiwa washtakiwa wote wanne walikula njama za kutenda kosa la kumjeruhi aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, ili kuleta hofu kwa Watanzania.

Mshtakiwa wa nne, Mbowe, anadaiwa katika shtaka la tatu, kwenye mikoa ya Morogoro na Dar es Salaam, alitoa fedha kwa washtakiwa wengine, akijua zitatumika kwa ajili ya kuwapata wahusika kwa ajili ya kulipua vituo vya mafuta Mwanza, Dar es Salaam na Arusha kwa lengo kuleta madhara kwa Watanzania.

Shtaka la nne kwa washtakiwa wote kwa pamoja wanadaiwa katika maeneo ya Aishi Hoteli, Kilimanjaro, Dar es Salaam, Morogoro, Arusha, walishiriki kikao cha nia ya kupanga ugaidi na wanadaiwa walipanga kulipua vituo vya mafuta, mikusanyiko ya watu na vitendo hivyo vililenga kuleta hofu na madhara kwa raia.

Katika shtaka la tano, mshtakiwa wa pili, Kasekwa, inadaiwa Agosti 5, 2020 akiwa Rau madukani, alikutwa na bastola aina ya Ruger A 5340 na ilikuwa na risasi tatu na ililenga kusaidia utendaji wa vitendo vya ugaidi kwa kulipua vituo vya mafuta na mikusanyiko Dar es Salaam, Morogoro na Arusha.



Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda (kulia), akiwa katika mazungumzo na Waziri wa Elimu Zanzibar, Simai Mohamed Said, jijini Dar es Salaam jana, ambapo walikubaliana kufanya kazi kwa karibu katika kupitia sera ya elimu na mitaala ya elimu msingi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

## Asilimia 80 ya sheria zatafsiriwa Kiswahili

Na Augusta Njoji, DODOMA

WAZIRI wa Katiba na Sheria, George Simbachawene, amesema asilimia 80 ya sheria zilizokuwa zikitumika mahakamani kwa lugha ya Kiingereza, zimetafsiriwa kwa Kiswahili.

Simbachawene alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kuhusu kikao cha 49 cha Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu alikichofunguliwa Februari 28, mwaka huu, na yeye alihutubia Baraza hilo juzi kwa njia ya video.

Kwa mujibu wa Simbachawene, kati ya sheria 450 zilizokuwa zikitumika mahakamani kwa Kiingereza, tayari 300 zimetafsiriwa kwa Kiswahili.

"Suala la kutafsiri sheria hizi linaenda vizuri. Hata kama kuanza kuzitumia linahitaji kukaa pamoja na mahakama ili kukubaliana lini zianze kutumika rasmi katika mhimili wa mahakama kwa lengo la kusaidia wananchi kupata haki kutokana na kutumika Kiswahili katika kutoa uamuzi au hukumu," alisema.

Akizungumzia kikao hicho, Waziri Simbachawene alisema Tanzania inatambua wajibu wake mkuu wa kulinda na kukuza haki za binadamu.

Simbachawene alisema serikali iko imara na inafanya jitihada za makusudi kuhakikisha haki za msingi na uhuru wa kidemokrasia, haki za kiraia na za kisiasa zinaheshimiwa na pia kuna mazingira wezeshi ya kukuza haki za kisiasa nchini.

"Rais Samia Suluhu Hassan alifungua kikao cha majadiliano Desemba, mwaka jana, baina ya viongozi wa juu serikalini na wa vyama vya siasa na wadau wa utawala bora na demokrasia nchini ikiwa ni kuhakikisha haki za msingi na uhuru wa demokrasia zinaendelezwa nchini," alisema.

Pia alielezea hatua madhubuti zilizochukuliwa na serikali katika kupambana na UVIKO-19 na kuifanya nchi kupata mkopo nafuu wa Sh. trilioni 1.3 wa kupunguza makali ya athari ya ugonjwa huo katika sekta mbalimbali zikiwamo za afya, elimu, maji na katika makundi ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

# Mwinyi aitwisha mzigo TCB kuinua wanawake kiuchumi

Na Rahma Suleiman, ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, amesema kuwa serikali anayoiongoza lengo lake ni kuubadilisha uchumi wa Zanzibar na kwamba wadau wa benki kama ya Biashara Tanzania (TCB) wanahitajika katika kufanya kazi pamoja hasa katika kuwainua wanawake kiuchumi.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana wakati alipokutana na kufanya mazungumzo na uongozi wa TCB, Ikulu ukiongozwa na Mkurugenzi Mkuu wa benki hiyo, Sabasaba Moshingi.

Alisema kwamba kusaidia wanawake ni jambo muhimu na Zanzibar kuna kundi kubwa la wajasiriamali ambao wengi wao ni kina mama ambao wanatakiwa kuungwa mkono hasa wanaojishughulisha na ukulima wa mwani.

Vile vile, alisema Serikali ya Zanzibar iko tayari kufanya kazi pamoja na benki hiyo na kumekuwa na mambo mawili ambayo yakiwakwaza wajasiriamali likiwamo dhamana pamoja na riba na ndiyo maana imeamua kwa makusudi kuingia makubaliano na benki ili kuwasaidia.

Alisema wakopaji wengi walikuwa hawana elimu ya kukopa ndiyo maana siku za nyuma walikuwa wakiuziwa mali zao za thamani na kusababisha kuwa na woga na serikali imeamua kulibeba na kuwachukulia dhamana wakopaji.

Alisema hatua hiyo itasaidia kuongeza ajira na walio wengi watajiingiza katika sekta ya uvuvi.

aliipongeza TCB kwa kutoa mikopo yenye thamani ya Shilingi bilioni tatu kwa wanawake wafanyabiashara wadogo Zanzibar na kusisitiza haja ya benki hiyo kuongeza kiasi hicho cha fedha ili mikopo hiyo iwafaidishe walio wengi. Alisema kwamba kuwapo kwa kongamano la wanawake Zanzibar, linalotarajiwa kufanyika Machi 5, mwaka huu 2022 lenye kaulimbiu ya 'Nafasi ya Mwanamke katika kukuza uchumi wa buluu kwa maendeleo endelevu', kutasaidia kuimarisha sekta za uchumi huo ikiwamo uvuvi, kilimo cha mwani pamoja na ufugaji wa samaki hasa kwa kinamama.

Alipongeza hatua ya benki hiyo ya kutoa mikopo inayokwenda sambamba na mafunzo ambayo yatasaidia shughuli zao za ujasiriamali. Aidha, Dk. Mwinyi alitoa pongezi kwa misaada iliyotolewa na benki hiyo kwa ajili ya Taasisi, vikundi vya kina mama wajasiriamali wanaojishughulisha na ukulima wa mwani na uchimbaji visima hatua ambayo itasaidia kuwaendeleza wanawake.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TCB, Moshingi alimpongeza Rais Mwinyi kwa maono yake ya uchumi wa buluu hatua itakayosaidia kukuza uchumi wa Zanzibar.

Alieleza matumaini yake ya maendeleo makubwa yatakayofikiwa Zanzibar kutokana na mikakati madhubuti iliyowekwa na serikali.

Alisema TCB ni benki kongwe yenye miaka 97 tangu ilipoanzishwa na kupitia mabadiliko mbalimbali makubwa na mwanzo ilijulikanwa kama TPB (Tanzania Postal Bank).

Alieleza jinsi ya umiliki wa benki hiyo hivi sasa na Serikali ya Zanzibar ina hisa zake na imekuwa na meneja wake anayefanya kazi Unguja na Pemba.

Pia, alisema benki hiyo imepitia mapinduzi makubwa na hivi sasa imeimarika kwa kiasi kikubwa ina matawi 82 kutoka 30 na wafanyakazi 1,001 ambayo inawalenga wananchi wa kawaida na wakubwa.

Alisema kwamba mnamo mwaka 2018 ilianzisha Benki ya Wanawake ambayo ilipata changamoto ya uendeshaji na hivi sasa imo ndani ya benki hiyo na tayari imeshaanza kutoa huduma na kufungua matawi kadhaa nchini na imetoa mikopo yenye thamani ya Sh. bilioni 127 na kwa upande wa Zanzibar tayari imeshatoa Shilingi bilioni tatu.

Alisema kuwa kuwapo kwa makongamano yaliyoanza katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma na kwengineko kutasaidia kutunza kumbukumbu, faida na mafunzo mengine ambayo kina mama wamepata mafanikio. Pia, alieleza misaada anayotarajia kuitoa kwa wajasiriamali siku ya kongamano hilo.

Kwa upande wake Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said alieleza haja kwa Benki hiyo kufanya kazi na Taasisi ya 'Zanzibar Maisha Bora Foundation' kwa ajili ya kuwasaidia kina mama wanaojishughulisha na ukulima wa zao la mwani kwa kuwa taasisi hiyo imelenga kuwasaidia wajasiriamali hao.

## Jela miezi 18 kuua kwa mkuki

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita imemhukumu Baraka Hamisi (40) kifungo cha miei 18 jela kwa kosa kumuua John Mathayo bila kukusudia kwa kumchoma na mkuki tumboni na kufariki dunia papo hapo.

Mshtakiwa huyo alipandishwa kizimbani mbele ya Jaji Peter Dyansobera na aliposomewa shtaka lake, alikiri kuhusika na kosa hilo.

Upande wa mashtaka ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Serikali Winfrida Mpiwa na utetezi ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Kujitegemea Penina Mashimba ambaye alikuwa akimtetea mshtakiwa huyo.

Jaji Dyansobera alisema baada ya mshtakiwa kukiri kosa lake, alimwambia Wakili wa Serikali amsomee maelezo ya awali.

Akisoma maelezo hayo, Mpiwa alidai kuwa Aprili 6, 2016 majira ya 1:00 kundi la watu wanaodaiwa kuwa majambazi lilivamia nyumba ya Mwanalingwa Mkitako na wakiwa wanaendelea kubomoa, Mwanalingwa alipiga kelele na watu hao wakakimbia na kuacha shoka likiwa na damu pamoja na ndoo ya maji.

Alidai kuwa wananchi walifika eneo la tukio na kuona lile shoka na kulitambua kuwa ni la John Mathayo ambaye kwa sasa ni marehemu.

Mpiwa alidai kuwa baada ya kulitambua lile shoka, walikwenda moja kwa moja hadi nyumbani kwa Mathayo na kumchukua hadi uwanja wa mpira kwa ajili ya mahojiano na wananchi waliongezeka wakiwa na silaha za jadi kama fimbo, mapanga na mikuki na walimuuliza kama shoka hilo ni lake ujibu ndiyo lakini hakuwapo katika uvunjaji wa nyumba ya Mwanalingwa.

Alidai kuwa baada ya Mathayo kukiri kuwa shoka ni lake, wananchi walimshambulia kwa kumpiga sehemu mbalimbali za mwili wake na wakati wakiendelea kufanya hivyo, Hamisi alimchoma na mkuki tumboni na kufariki dunia papo hapo.

Baada ya hapo, alidai kuwa askari polisi walifika eneo la tukio na kumkamata Hamisi na kumpeleka kituo cha polisi Geita na alipohojiwa kuhusiana na tukio hilo alikiri kumchoma mkuki tumboni Mathayo.

Baada ya Wakili Mpiwa kumaliza kumsomea maelezo ya awali, Jaji Dyansobera alimuuliza mshtakiwa kama maelezo hayo ni ya kweli na kujibu kwamba ni ya kweli ndipo akamtia hatiani na kumtaka ajitetee.

Mshtakiwa huyo akiongozwa na Wakili Mashimba, aliomba mahakama impunguzie adhabu kwa kuwa ana familia zinawategemea, pia mteja wake amekaa mahabusu kwa miaka sita hadi sasa.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Mpiwa uliomba mahakama itoe adhabu kwa mujibu wa sheria. Jaji Dyansobera alitupilia mbali ombi la utetezi na kusema kila mtu anatakiwa avune kile alichopanda.

"Mshtakiwa hukuwa na sababu ya kumchoma mkuki marehemu kwa sababu nyumba iliyokuwa ikivunjwa ilikuwa si yako. Sasa utatumikia kifungo cha mwaka mmoja na nusu jela na upande ambao haujaridhika na uamuzi huu rufani iko wazi," alisema.

# Mfalme Zumaridi afunguliwa kesi tatu

**Richard Makore na Rose Jacob,** MWANZA

BAADA ya kushikiliwa kwa takribani siku saba na polisi, Mchungaji Diana Bundala, maarufu kama Mfalme Zumaridi, na wenzake 92 wamefikishwa katika Mahakama ya Hakimu Mkazi ya Mkoa wa Mwanza na kusomewa mashtaka matatu.

Mashtaka hayo ni pamoja na kushambulia polisi, kuzuia polisi kufanya kazi yao na kusafirisha binadamu ambalo linamkabili Zumaridi peke yake. Washtakiwa hao walifikishwa mahakamani zikiwa ni siku saba tangu walipokamatwa nyumbani kwa mchungaji huyo, Buhongwa jijini Mwanza.

Katika mahakama hiyo, ulinzi wa polisi uliimarishwa na ilipotimia saa 9.14 alasiri, magari matatu ya polisi yaliyawashusha washtakiwa hao.

Mchungaji huyo ambaye ana wafuasi wengi katika kanisa lake jijini hapa, alionekana mahakamani hapo mwenye furaha na kunyosha juu mkono wake mmoja ukiwa na majeraha ya kupigwa.

Washtakiwa wote 93 walisomewa mashtaka yao na waendesha mashtaka wa serikali, Hemed Khalid na Emmanuel Luvinga na walikana baada ya kuulizwa kama ni kweli.

Waendesha mashtaka waliiambia mahakama kwamba kesi hiyo Na. 10 ya mwaka 2022 inamhusu Mchungaji Bundala na wenzake wanane ambao wanadaiwa kufanya shambulio la kudhuru mwili na kuzuia maofisa wa polisi kufanya kazi.

Aidha, walidai kuwa kesi Na. 11 ya mwaka 2022, inamhusu Zumaridi peke yake ambayo ni usafirishaji haramu wa binadamu wakati kesi Na. 12 ya mwaka 2022 inamhusu Zumaridi na wenzake 84 wanaodaiwa kufanya kusanyiko lisilo halali.

Wiki iliyopita, watuhumiwa hao walikamatwa nyumbani kwa mchungaji huyo na jeshi la polisi mkoani Mwanza na kushikiliwa hadi jana walipofikishwa mahakamani.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Mwanza, mwishoni mwa wiki iliyopita, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Ramadhani Ng'anzi, alisema mtuhumiwa huyo alikamatwa nyumbani kwake akiwa na watu 149 waliokuwa wakiishi kwake.

**WAGOMA DHAMANA**

Katika hali isiyokuwa ya kawaida, washtakiwa 91 waliokamatwa na Zumaridi, waligoma kudhaminiwa katika kesi inayowakabili ya shambulio la mwili na kuzuia polisi kufanya kazi yao.

Washtakiwa hao walidai kuwa hawako tayari kudhaminiwa na kumwacha mchungaji wao ambaye kosa lake la kusafirisha binadamu kutokuwa na dhamana.

Baada ya Zumaridi kukosa dhamana, wenzake ambao ni wafuasi wake, walikataa kudhaminiwa kwa madai kwamba wako tayari kufa naye pamoja gerezani.

Wakili wa washtakiwa, Eric Mutta, baada ya kuahirishwa kesi, alidai kuwa wateja wake 91 ambao dhamana zao zilikuwa wazi wamekataa kudhaminiwa kwa madai kwamba wako tayari kufa na mama yao (Zumaridi) ambaye anajiita Mungu.

Kesi hiyo inatarajiwa kutajwa Machi 17, mwaka huu, na washtakiwa 92 wamepelekwa rumande katika Gereza la Butimba.



Meneja wa Mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM), Zilipa Mgeni (kushoto), akikabidhi msaada wa sehemu ya nguruwe 160 kwa wawakilishi wa vijana 80 wanaoishi katika mazingira magumu kutoka kata tatu za Luhunga, Mdabulo na Ihanu, wilayani humo mkoani Iringa jana, ambao wapo kwenye mradi huo, kama mtaji wa kujikwamua kiuchumi. Wa (tatu kushoto) ni Kaimu Mtendaji wa Kata ya Luhunga, Vumilia Nyunza. **PICHA: FRANCIS GODWIN**

# Adaiwa kuua mke, mtoto kisha kujiua

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKAZI wa Kijiji cha Bulambila wilayani Shinyanga, Madirisha Kanyalu (60) amefariki dunia kutokana na kinachodaiwa kujitumbukiza kwenye dimbwi la maji muda mfupi baada ya kumuua mke wake, Evodia Nyerere (27), na mtoto wake, Meshack (miezi 11).

Akizungumza na waandishi wa habari kuhusu tukio hilo jana mjini hapa, Kaimu Kamanda wa Polisi mkoani Shinyanga, Joseph Paul, alidai Kanyalu aliwaua mke na mtoto wake kwa kuwakata na kitu chenye ncha kali shingoni.

Kaimu Kamanda Paul alisema tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa 12 asubuhi katika nyumba waliyokuwa wanaishi.

Alidai kuwa Kanyalu baada ya kutekeleza mauaji hayo, alikwenda kujitumbukiza kwenye dimbwi la maji lililoko karibu na nyumba yake na kufariki dunia.

"Chanzo cha tukio hilo ni mgogoro wa kifamilia, kwamba mwanaume huyo alikuwa akimtuhumu mke wake kuwa na uhusiano na wanaume wengine," alisema Kaimu Kamanda Paul.

Alisema miili ya marehemu hao wote imekabidhiwa kwa ndugu zao kwa ajili ya mazishi.

Kaimu Kamanda Paul alitoa wito kwa wanandoa mkoani humo kuwa na utaratibu wa kupeleka malalamiko yao mapema kwenye Dawati la Jinsia la Jeshi la Polisi na Ustawi wa Jamii ili kupata suluhisho la migogoro yao badala ya kujichukulia sheria mkononi na kusababisha mauaji.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mikopo halmashauri iinue kinamama kwenye kilimo

**MPANGO** wa Chakula Duniani WFP katika moja ya taarifa zake unathibitisha kuwa wanawake wa Ukanda wa Afrika Kusini ya Jangwa la Sahara ndiyo wazalishaji wakubwa wa chakula.

Ndiyo wanaolima takribani asilimia 80 ya vyakula mbalimbali vinavyoliwa katika eneo hilo na hata kuuzwa nje.

Licha ya kinamama kuwa wazalishaji wakubwa wa chakula hapa Tanzania na kwingineko Afrika, suala la kuwa na ardhi wanayoimiliki kwa majina yao bado ni changamoto.

Ndiyo maana tunaamini kuwa kuwapo kwa asilimia 10 ya fedha za halmashauri zinazotolewa kwa wanawake, vijana na wanaoishi na ulemavu kutakuwa na tija zaidi kama tutahakikisha kuwa kinamama wanamiliki ardhi kwa majina yao.

Kwa kuangalia eneo hilo, tunaamini ni wakati wa kuwezesha asilimia 10 ya fedha za halmashauri inayotolewa kwa wanawake, vijana na wenye ulemavu inavyoweza kutumika kikamilifu kuwekeza kwenye kilimo.

Mahitaji ya mboga, matunda na chakula ni makubwa mno ndani ya nchi iwe mijini na vijijini, lakini hata nje ya mipaka hivyo, kinamama wana fursa kubwa

Tukumbuke kuwa kumiliki ardhi kutawawezesha kupanga na kufanya uzalishaji kwa uhakika zaidi badala ya kutegemea kukodisha . Wanawake wengi mfano mkoa wa Mbeya, Songwe, Morogoro na Pwani wanakodisha ardhi kwa kilimo.

Inamaanisha kuwa kama wangekuwa na mashamba yao pekee huenda wangekuwa mbali zaidi kwenye uzalishaji wa chakula na mazao ya biashara, ufugaji pamoja na uvuvi.

Tukiwaweka pamoja wanawake na vijana, tunaona kuwa wengi wanashindwa kujikita moja kwa moja kwenye kilimo kwa kutumia fedha za halmashauri za asilimia 10.

Ukweli ni kwamba mikopo hiyo imetumiwa zaidi kwenye biashara kama ya kuuza vyakula (mama lishe), nafaka, matunda na mboga na wengine kufuga kuku.

Wapo wanaojikita kwenye biashara za urembo kama saluni, mavazi , shuka na wengine wakiwekeza kwenye maduka yakiwamo ya kuuza vyombo vya nyumbani na kilimo japo kwa kiwango kidogo.

Ni wazi kuwa ardhi inayomilikiwa kwa pamoja na familia,wana ndugu au ukoo siyo rahisi kijana au mwanamke akaipata na kuitumia kuzalisha bila kufuata mlolongo mrefu ambao pia unatawaliwa na mfumo dume ndani ya familia, jamii na hata mfumo mzima wa ardhi.

Licha ya kwamba hatuna takwimu sahihi , ukweli unabakia kuwa asilimia kubwa ya ardhi ya Tanzania inamilikiwa na wanaume na huenda wanawake wana asilimia mbili pekee na iliyobakia 98 inamilikiwa na wasio wanawake.

Hata hivyo, huu siyo wakati wa kugombea umiliki ila tunachoshauri ni halmashauri nchini ziangalie, uwezekano wa kuanzisha kanda za ardhi ya kilimo kwa kutenga maeneo mahsusi na kuyakodisha kwa masharti nafuu ili wanawake wayatumie kwa kilimo cha mboga, matunda na mazao mengine kwenye halmashauri au wilaya mbalimbali.


Kama ambavyo halmashauri zinatenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji (special economic zones) ni vyema kutenga ardhi kwa ajili ya uwekezaji kwenye kilimo kwa ajili ya wanawake hasa wanaokopa mikopo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri ili waitumie kwenye kuzalisha chakula, mboga na matunda na kuwainua au kuwawezesha zaidi kupitia kilimo wakipitia mikopo ya halmashauri.

Wanawake hawawezi kutumia mali za familia kama ardhi na kuwekeza kama wanavyotamani, ikumbukwe kuwa wanawake hawana haki ya kumilika ardhi na kuzitolea maamuzi hata waume zao wakiwapo na iwapo wenzao hao wamefariki wanakuwa na wakati mgumu.

Ni kwa sababu ni mali ya familia nzima hivyo mama mjane, hawezi kufanya maamuzi ya ardhi ya marehemu mumewe kwa kufanya kile anachopenda hasa kuweka vitega uchumi.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Dunia duara, vita vilivyoko ughaibuni vinatuhusu tuliko

Na Christina Mwakangale

**DUNIA** pamoja na nchi moja au nyingine kuwa na tofauti za umbali wa maelfu ya maili na kijiografia, hilo halimaanishi hatutegemeani.

Unapokuja katika masuala mbalimbali ya kimataifa, kidiplomasia, kiuchumi, kisiasa na kijamii utabaini dunia ni kitu kimoja.

Anza kuangalia namna viwanda na bidhaa zake ambazo zinatengenezwa na kusambaa duniani kote, mfano magari, televisheni, simu, kompyuta, nguo za dukani na mtumba na vyakula mbalimbali vinaingia na kutoka mabara yote saba.

Afrika, tukiwa sehemu ya dunia pamoja na kwamba hatujainuka zaidi kiuchumi hasa kusini mwa jangwa la Sahara, kama nchi zilizoendelea tunategemewa kutoa malighafi zinazotegemewa uko nchi za mbali zitokanazo hasa shambani.

Bidhaa hizo zinahitaji kukusanywa huko zinakolimwa zaidi yaani vijijini na kisha kuletwa mjini, ukiangalia kinachohitajika ni usafiri wa vyombo vya moto ambavyo hutumia mafuta iwe dizeli au petroli.

Ndio maana linapokuja suala la mgogoro hasa vita athari zipo za moja kwa moja na ambazo si za moja kwa moja, na kusababisha uchumi kuyumba.

Vita inapotokea jambo la kwanza ambalo litaanza kuiumiza Afrika ni kupanda kwa bei za mafuta.

Baada ya Russia kuanzisha mashambulizi dhidi ya Ukraine, bei ya mafuta ikapanda kufikia kwenye soko zaidi ya dola 100 kwa pipa moja.

Kiwango hicho ni kikubwa zaidi cha kupanda kwa bei tangu ilipotokea mwaka 2014.

Katika eneo la Afrika Mashariki, Kenya itapata pia athari za kiuchumi kwa kuwa ni mwagizaji mkuu wa ngano, kutoka Russia.

Pia Kenya katika ukanda huu ni muuzaji mkubwa wa chai kwenda Russia.

Mwaka jana pekee, Kenya iliuza chai yenye thamani ya shilingi za Kenya bilioni 6.2 kwa kipindi cha kati ya Januari hadi Novemba, lakini biashara hiyo sasa inaingia mashakani kutokana na vita hiyo.

Masuala ya kijeshi, Diplomasia na Usalama kwa Afrika pia yanaweza kuyumba kutoka na vita Russia na Ukraine, na kuiweka Afrika katika nafasi ngumu kwenye uhusiano wake na nchi kubwa duniani. Ingawa inaonekana kama ni mgogoro baina ya nchi mbili.

Ni kwamba hivi karibuni Russia imeanza kujitanua Afrika na imeanza kutoa misaada ya kijeshi kwa nchi za Afrika, kuanzia eneo la Mashariki, Pembe ya Afrika na Afrika ya Kati.

Maeneo hayo ni Sudan, Somalia, Sudan Kusini, Mali, Msumbiji na kwingineko ambako kulianza kutazamwa kwa kina, sasa kutapunguzwa umuhimu wakati jamii ya kimataifa ikitazama Ukraine.

Russia ni miongoni mwa wasambazaji wakubwa wa nishati ya gesi na mafuta duniani na mgogoro huu utaathiri uzalishaji wake ama kwa vikwazo ambavyo tayari vimewekwa na taifa moja kama vile Marekani na Uingereza pamoja na Umoja wa Ulaya (EU).

Afrika tayari inapitia katika kipindi kigumu kiuchumi. Wiki iliyopita, ni wazi kupanda kwa bei ya mafuta kutaongeza bei zaidi ya bidhaa mbalimbali na kufanya hali kuwa ngumu zaidi.

Kupanda kwa bei ya mafuta huanzisha mnyororo wa kupanda kwa bei za uzalishaji na usafirishaji wa bidhaa.

Tatizo kubwa zaidi kiuchumi ni kwamba sasa nchi zitalazimika kutumia fedha nyingi zaidi za kigeni kuagiza mafuta kuliko kawaida na hili huathiri akiba ya fedha za kigeni ya nchi na kupunguza matumizi ya ambayo ingetumika kwenye mambo mengine.

Russia na Ukraine ndiyo wasambazaji wakuu wa ngano na mazao mengine ya nafaka duniani.

Misri, nchi yenye watu wengi na ushawishi mkubwa zaidi katika eneo la Kaskazini mwa Afrika ndiyo mwagizaji mkuu wa ngano duniani.

Ngano ni muhimu kwa taifa hilo kiasi kwamba waandamanaji waliomng'oa madarakani Rais Hosni Mubarak, walikuwa wakilila zaidi mambo mawili tu; mkate na uhuru.

Tayari Mpango wa Chakula Duniani (WFP) umeonya kwamba mgogoro huo utaathiri bei za vyakula na kusababisha njaa kwa maskini katika eneo la Kaskazini mwa Afrika.

# Shule zafungiwa mtandao intaneti

**Na Romana Mallya**

KAMPUNI ya Liquid Intelligent Technologies imeanza kuzitambua shule za msingi na sekondari nchini ambazo hazina huduma ya mtandao (internet) ili iweze kuziunganisha bure kuanzia mwezi Mei, mwaka huu.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, inayojihusisha na huduma za kidigitali, Denny Marandure, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam na kueleza kuwa lengo ni kuwaongezea uelewa wanafunzi wa kufanya utafiti kulingana na masomo wanayojifunza.

Alitoa kauli hiyo wakati kampuni hiyo ikizinduliwa kutoka jina la Raha Liquid Telecom na sasa inatambuliwa kama Liquid Intelligent Technologies.

"Tunataka wanafunzi waweze kupata huduma za mtandao wawapo shuleni ili ziwasaidie katika masomo yao, kwa sasa tunaanza kwa kuzitambua shule hizi nchini na mwezi Mei, mwaka huu tutaanza kuzifungia huduma ya mtandao bure," alibainisha.

Alisema mabadiliko ya teknolojia yamefanya wanafunzi wanapotaka kujifunza zaidi hukimbilia mtandao badala ya maktaba kama ilivyokuwa hapo awali.

"Mtu anapoamka asubuhi hitaji la kwanza siyo chai ni mtandao ili afungue simu yake aangalie huko atafanya mihamala ya kifedha na mambo mengine," alisema.

Marandure alisema pia ameshauri kampuni kubwa na ndogo kutumia mfumo imara wa kiusalama wa kimtandao ili kulinda taarifa za kibiashara kwenye mfumo mzima wa ufanyaji shughuli zao.

Alisema kwa miaka miwili Liquid imejiimarisha kama kampuni ya kiafrika inayotoa huduma za mindombinu ya kidigitali ikiwa ni mtandao unaozunguka zaidi ya kilometa 100,000.

Alisema imekuwa ikiamini kuwa ushirika baina ya taasisi binafsi na za umma ni muhimu kwa maendeleo ya kiuchumi.

"Tunatarajia kushirikiana na serikali kuisaidia kuyafikia kwa ukamilifu malengo iliyojiwekea ambayo ni msingi wa mafanikio ya muda mrefu ya Tanzania," alisema.

Alisema wao kama mshirika wa Microsoft Gold, wanazipambanua upya huduma za kiuunganishaji, kimtandao na usalama mtandaoni kupitia ushirika wa kimkakati na kampuni ili kuleta ubunifu kwenye ufanyaji biashara, huduma za kisasa na usalama.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa kampuni hiyo, Adil Youssefi, alisema wamefanya mabadiliko hayo ili kuleta huduma zote kuwa za mtandaoni kwa mfumo wa kompyuta, usimamizi wake na suluhusho la usalama wa kimtandaoni.

# Waziri ataka mipaka vijiji iheshimiwe

**Na Waandishi Wetu,**
CHALINZE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, ametaka mipaka ya ardhi baina ya kijiji na kijiji iheshimiwe ili kuepuka migogoro. Amesema mipaka ya vijiji imewekwa ili kuwezesha utoaji bora wa huduma kwenye jamii husika na wananchi hawapaswi kugombania rasilimali ardhi hiyo.

Ridhiwani ambaye ni Mbunge wa Chalinze, alisema hayo juzi alipoanza ziara ya kusikiliza na kutolea ufafanuzi changamoto mbalimbali katika jimbo lake ikiwamo migogoro ya ardhi.

Katika siku ya kwanza ya ziara yake, alitembelea kata ya Miono na kufanya mikutano kwenye vijiji vya Kweikonje, Masimbani na Miono mjini.

"Kila Mtanzania ana haki ya kumiliki ardhi sehemu yoyote nchini lakini kwa watu wanaotoka nje ya kijiji husika, wanapaswa kufuata sheria na taratibu ikiwamo kuwasilisha maombi ofisi ya kijiji na baada ya hapo mkutano mkuu wa kijiji uitishwe ili kijiji kiridhie kumpa ardhi hiyo mwombaji," alisema.

Kauli hiyo ya Ridhiwani inatokana na taarifa za mwananchi mmoja kutoka mkoa mwingine anayeishi kijiji cha Masimbani kuomba kibali cha kumiliki ardhi katika kijiji hicho na kuishia kuzungushwa na uongozi wa kijiji.

Katika kikao hicho, ilionekana pia kuna migogoro mingi kati ya wafugaji na wakulima sambamba na migogoro ya mipaka na Kamishna wa Ardhi Msaidizi Mkoa wa Pwani, Lucy Kabyemera, alisema kila kijiji lazima kipimwe ili mpango wa matumizi bora ya ardhi uandaliwe kwa kuwa utasaidia kuepusha migogoro ya ardhi.

"Kwa kukamilisha upimaji haraka itasaidia kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi na kila aliyepimiwa ana haki ya kuandaliwa hatimiliki ya kimila itakayomuhakikishia usalama wa milki yake. Katika upimaji huo elimu pia itatolewa ili wananchi wajue umuhimu wa kupata hati kwenye maeneo wanayoishi," alisema Kabyemera.

Mmoja wa wananchi waliohudhuria mikutano hiyo, aliyejitambulisha kwa jina la Kawambwa, alisema wananchi wanahitaji kupimiwa maeneo yao ili kupata hati ambazo zitawasaidia kupata mikopo aliyosema itasaidia kuongeza nguvu kwenye biashara zao.

Kupitia mkutano huo, wananchi wa Kata ya Maono walisisitizwa pia kutoa ushirikiano, kujitokeza kwa wingi pamoja na kutoa taarifa sahihi kwenye mpango wa anwani za makazi unaotarajiwa kuanza mapema mwezi huu na kwamba vijana kwenye mitaa watatumika kukusanya taarifa hizo.




Ofisa Kitengo cha Kadi Benki ya NMB, Lightness Zablon, akionyesha mashine ya malipo na kadi, wakati wa kuchezesha droo ya tisa ya Kampeni ya 'NMB Mastabata Kivyako Vyako', jijini Dar es Salaam jana. Kulia ni Ofisa Huduma kwa Wateja, Suzan Manga na (kushoto) ni Msimamizi kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Elibariki Sengasenga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shirika laingia majumbani kuhimiza chanjo UVIKO-19

**Na Sabato Kasika**

SHIRIKA lisilo la kiserikali la Eden Twins Foundation linalotoa huduma za kijamii kwa wazazi wenye watoto mapacha wasio na uwezo kiuchumi, limeanza kuhamasisha chanjo ya UVIKO-19 kwa wazazi hao.

Mwenyekiti wa shirika hilo, Diana Mbena, ameliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana kuwa, anahamasisha chanjo anapotembelea wazazi hao majumbani mwao kwa lengo la kuwajulia hali.

Alisema, makao makuu ya shirika hilo yapo Kibaha mkoani Pwani, na kwamba, amekuwa akitembelea wazazi wa mkoani humo na Dar es Salaam akiwatia moyo kuhusu magumu ya maisha wanayopitia, na kuhimiza chanjo.

"Nimeona kuwa hiyo ndiyo njia rahisi ya kufikisha ujumbe kwa wanachama wa Eden Twins Foundation kwa kuwa shirika hili bado ni changa, halijapata nyenzo za kutosha za kufanyia kazi," alisema Diana.

Alisema, tangu chanjo ianze kutolewa, amekuwa akishuhudia mashirika na taasisi mbalimbali zikishiriki kwenye kampeni za kuhamasisha chanjo katika maeneo mbalimbali yakiwamo ya wazi.

"Nami kwa kuwa shirika langu bado ni changa, nimeamua kutumia ziara za kutembelea wazazi majumbani mwao kuwajulia hali, na pia kuhimiza muhimu wa chanjo ili waamue kuchukua hatua, kwani swala la chanjo ni la hiari," alisema.

Alisema, yeye ni miongoni mwa Watanzania waliopata chanjo mapema mara tu baada ya kuzinduliwa na Rais Samia Suluhu Hassan mwishoni mwa Julai mwaka jana, na kwamba hana budi kuhamasisha wengine.

"Katika ziara zangu katika nyumba mbalimbali zenye watoto mapacha, kuna baadhi ya vitu ambavyo nimebaini hasa pale ninapogusia suala la chanjo, kwani wapo wanaoamini kuwa chanjo hiyo si salama," alisema.

Alisema, hali hiyo inaonyesha kuwa elimu zaidi inahitajika kutoka kwa wataalamu wa afya, kwa madai kwamba, watu wanataka kuelimishwa kuhusu muhimu wa chanjo, waelewe ndipo wachukue hatua.

Diana alisema, yeye si mtaalamu wa afya, lakini kama mwenyekiti wa shirika hana budi kutoa hamasa kwa wanachama wa Eden Twins Foundation ili watu wajitokeze kwa wingi kupata elimu, hatimaye waamue kuchanja.

"Ninaamini kwamba, jamii imepotoshwa sana kuhusu chanjo, hivyo wakati kukiwa na uhamasishaji, wataalamu wa afya nao kwa upande wao wajitokeze kwa wingi kutoa elimu sahihi," alisema.

Alisema hatua hiyo inaweza kusaidia Watanzania wengi kutoka kwenye giza na kuamua kwenda kwenye vituo vya chanjo ili kupata huduma hiyo ambayo inaendelea kutolewa kote nchini.

# Wanafunzi 84 wakatisha masomo kwa ujauzito

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

WANAFUNZI 84 mkoani Shinyanga wameripotiwa kupewa ujauzito, hivyo kukatisha masomo wakiwamo 27 kutoka shule za msingi na 57 sekondari.

Ofisa Elimu Mkoa wa Shinyanga, Dafroza Ndalichako, alibainisha hayo jana kwenye kikao cha wadau wa elimu mkoani hapa wakati akisoma taarifa ya elimu ya mkoa.

Alisema katika mkoa huo kumekuwa na changamoto kubwa ya wanafunzi kushindwa kuhitimu masomo yao kutokana na kukabiliwa na vikwazo mbalimbali, vikiwamo utoro na wanafunzi wa kike kupewa ujauzito.

"Mkoa wetu wa Shinyanga tumekuwa tukikabiliwa na tatizo la wanafunzi kushindwa kuhitimu masomo yao kutokana na sababu mbalimbali ikiwamo ya utoro na wanafunzi kupewa ujauzito. Takwimu za mwaka jana zinaonyesha kuwa wanafunzi 27 wa shule za msingi walipewa ujauzito na 57 kutoka shule za sekondari," alisema Ndalichako.

Pia alisema takwimu zinaonyesha kuwa wanafunzi waliohitimu elimu ya msingi mwaka jana walikuwa 38,694, lakini walioandikishwa kuanza darasa la kwanza mwaka 2015 walikuwa 48,298. Kwa takwimu hizo, alisema wanafunzi 9,604 hawakumaliza elimu ya msingi kutokana na sababu mbalimbali zikiwamo utoro na mimba za utotoni.

Kwa upande wa shule za sekondari waliandikishwa wanafunzi 19,213 kuanza kidato cha kwanza mwaka 2018, lakini waliofanya mtihani wa kuhitimu elimu ya Sekondari kidato cha Nne mwaka jana ni 13,989, huku 5,224 hawa kuhitimu elimu hiyo

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Sophia Mjema, aliagiza watuhumiwa wote kwa mimba hizo za wanafunzi wachukuliwe hatua za kisheria ili liwefundisho kwa wengine na kutokatisha ndoto za wanafunzi. Pia aliagiza viongozi kwa ngazi zote za halmashauri mkoani hapa kuweka mikakati ya kuanza utoaji wa chakula cha mchana shuleni, ili wanafunzi wape chakula na kuacha kuwa watoro na kufanya vizuri kitaaluma.

Alionya pia tabia ya baadhi ya watu kupotosha kuwa elimu kwa sasa ni malipo na kubainisha kuwa bado inatolewa bure na kutoa wito kwa wazazi waendelea kuandikisha watoto wao kwa wingi na hatimaye kupata elimu ili kuwasaidia baadaye na kuwa tegemeo kwa taifa.

Mjema alisema hali ya uandikishaji wanafunzi kwa mwaka 2022 kwa elimu ya awali ni asilimia 88, msingi 97 na sekondari ni asilimia 83 na kwamba uandikishaji unaendelea hadi Machi 31, mwaka huu.



Mfanyakazi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), akisoma mita ya mteja eneo la Tabata mkoani humo juzi, wakati wa operesheni ya kukusanya madeni inayoendelea ambapo mamlaka hiyo imewataka wananchi kulipia huduma ya maji ili kuiwezesha kutoa huduma bora zaidi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi DAWASA wasisitizwa ufanisi

**Na Mwandishi Wetu**

WATUMISHI wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), wametakiwa kuthamini kazi ya kutoa huduma ya Majisafi na usafi wa Mazingira kwa wateja na kuitenda kwa ufanisi mkubwa.

Akizungumza katika kikao kazi cha wafanyakazi wote kilichofanyika juzi, Ofisa Mtendaji Mkuu wa DAWASA, Mhandisi Cyprian Luhemeja, alisema huduma ya maji ni muhimu, hivyo kila mtumishi anapaswa kufanya wajibu wake kwa uaminifu mkubwa.

"Sote tunapaswa kuelewa kwamba kufanya kazi katika sekta ya maji ni kwa kusudi maalum na si kwa bahati mbaya, hivyo kila mtumishi ana mchango sahihi katika kukuza maendeleo ya mamlaka," alisema Mhandisi Luhemeja.

Aliongeza kuwa kila mtumishi wa mamlaka ana jukumu la kutengeneza mazingira mazuri ya kuishi kwa wakazi wa Dar es Salaam na Pwani kupitia huduma ya majisafi kwa kuhakikisha upotevu wa maji unadhibitiwa ili kuboresha upatikanaji wa maji kwa wateja.

Luhemeja aliongeza kuwa udhibiti upotevu wa maji unasaidia mamlaka kuokoa mapato yanayokosekana ya kuwezesha kuboresha huduma.

Kikao kazi hicho ni cha kwanza tangu kuanza mwaka 2022 kilicholenga kufanya tathimini ya utendaji kwa mwaka uliopita.

# Ashauri usawa kijinsia udumishwe kwenye jamii

**Na Christina Haule,**
MOROGORO

USAWA wa kijinsia unapaswa kudumishwa ili kuendelea kuleta ustawi kwa maendeleo ya kesho kwenye jamii nchini na duniani.

Kaimu Naibu Kamishna wa Uhifadhi Wanyamapori, Utalii na Biashara kutoka Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Nyangabo-Violeth Mosika, alisema hayo wakati akiongea na waandishi wa habari kuhusu sherehe za Siku ya Wanawake Duniani, alisema kada hiyo kupata nafasi kwenye kazi mbalimbali za kijamii nchini ikiwamo za kijeshi, imeleta mabadiliko yenye neema na kuongeza uaminifu katika jamii

Nyangabo ambaye ni Ofisa Wanyamapori Mkuu daraja la kwanza, alisema kutokana na dhima ya siku ya wanawake mwaka huu inayozungumzia masuala ya jinsia, suala la kusema huyu ni mwanamke usimpe kazi fulani halipo na halipaswi kupewa nafasi kwa sababu yeye akiwa mwanamke hadi anafikia cheo alichonacho ametembea zaidi ya kilometa 15 kwa miguu doria porini akiwa na kundi la wanaume.

Alisema anapotaka kuingia kazini kama mhifadhi wanyamapori hana tofauti na wanaume bali anapaswa kujiandaa kwa kubeba silaha kwa ajili ya kulinda na kujilinda, vifaa vya mawasiliano kwa ajili ya kujua alipo na kumwongoza kama amepotea na pingu ya kumfunga jangili kama umemkamata.

"Mwanzoni kabisa walikuwa wanatuita, wee bwana nyama, bwana nyama, lakini mi ilini-wia vigumu kugeuka licha ya kwamba nipo kwenye kundi la wanaume lakini kwa sasa hali imebadilika tupo wanawake wengi, tunaosimamia shughuli za wanyamapori," alisema.

Alisema zamani ilijengeka dhana kuwa wanaume ndiyo wanaongoza na kufanya kazi mbalimbali tofauti na wanawake, lakini wanawake wanapaswa kusimama kwenye nafasi walizoko ili kuweza kufikia malengo yanayokusudiwa.

"Mimi nikiwa doria sitegemei mwingine niliye naye bali ni kazi yangu na kuonesha doria naweza na kusimamia matumizi endelevu ya kazi zangu, imenisaidia kunifikisha hapa, wapo watu waliodai si lazima mwanamke kuwa porini lakini si kweli ni wazi kwamba unapaswa kuwa porini na hata ofisini pia," alisema.

Nyangabo alisema mwanamke awe mjini au kijijini anatumia rasilimali zinazotokana na ikolojia za misitu kama vile kuni na maji ili kutekeleza majukumu yake ya kila siku nyumbani sambamba na kuwa na nafasi ya ulinzi wanyamapori hasa akiwa ameolewa na mhifadhi hivyo anapaswa kuyalinda na kuyahifadhi.

Maadhimisho ya sherehe hizo kitaifa hufanyika kila baada ya miaka mitano na mara ya mwisho ilikuwa mwaka 2020 na yalifanyika mkoani Simiyu na kimkoa kwa Mkoa wa Morogoro sherehe hizo zinatarajia kufanyika wilayani Ulanga.

## Mil. 140/- sasa zapata washindi NMB MastaBata

**Na Mwandishi Wetu**

JUMLA ya Sh. milioni 140 zimechukuliwa na washindi kati ya Sh. milioni 240 za kampeni ya NMB MastaBata.

Msimu wa tatu wa Kampeni ya NMB MastaBata inayoendeshwa na Benki ya NMB, umezidi kushika kasi kuelekea ukingoni baada ya jana kufanyika kwa droo ya tisa, ambako washindi 100 walijinyakulia Sh. milioni 10, hivyo kufanya pesa zilizopata washindi kufikia Sh. milioni 140 kati ya Sh. milioni 240 zinazoshindaniwa.

NMB MastaBata – Kivyako Vyako, ni kampeni inayohamasisha matumizi na manunuzi kwa njia ya kadi badala ya pesa taslimu, ambayo inaendeshwa kwa kipindi cha wiki 10, zitakazoshuhudia wateja 1,080 wakijishindia pesa taslimu Sh. milioni 240, wakiwamo washindi 1,000 wa wiki, washindi 50 wa mwezi na 30 wa 'Grande Finale.'

Akizungumza kabla ya uchezeshwaji wa droo hiyo jijini Dar es Salaam, Ofisa wa Kitengo cha Kadi wa NMB, Lightness Zablon, alibainisha kuwa kampeni hiyo imekuwa na mafanikio makubwa, kwani imeongeza idadi ya miamala ya matumizi kwa njia ya kadi za MasterCard, Mastapass QR, vituo vya Mauzo (PoS) na mtandaoni.

"Tayari wateja 850 wamejishindia zawadi ya pesa taslimu katika wiki nane zilizopita, pamoja na droo mbili za mwisho wa mwezi Januari na Februari. Na leo tunaenda kupata washindi wengine 100 wa wiki ya tisa, hivyo tumebakisha wiki moja (washindi wengine 100) na droo ya fainali ya washindi 30 mwishoni mwa mwezi huu.

"Kampeni imeonyesha mafanikio makubwa kwa kuwa imeongeza idadi ya miamala. Maana yake ni kwamba mwitikio wa matumizi ya kadi umekuwa mkubwa, kulingana na mahitaji ya kidijitali, ambako sasa unaweza hata kuagiza bidhaa nje ya nchini na kulipia kwa njia za kadi, badala ya pesa taslimu ambazo ni hatari kwa usalama," alisema.

Droo hiyo ilifanyika chini ya uangalizi wa ofisa kutoka Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Elibariki Sengasenga, ambaye aliwahakikishia wateja wa benki hiyo kwamba kampeni hiyo inafanyika kwa kufuata vigezo, kanuni na sheria zinazotambulika na bodi yake na kuwatoa shaka wateja juu ya upatikanaji washindi.

Wakati washindi 100 wa kila wiki wakijishindia Sh. 100,000 kila mmoja, washindi 25 wa droo ya mwisho wa mwezi wa NMB MastaBasta hujishindia Sh. milioni 1 kila mmoja, huku washindi 30 watakaopatikana kwenye 'grande finale' wakitarajia kujinyakulia Sh. milioni 3, hivyo washindi 1,080 watazoa Sh. milioni 240.

# Jela miaka 2 kwa kula njama kufanya mauaji

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MAHAKAMA Kuu ya Tanzania Kanda ya Mwanza iliyoketi Geita, imewahukumu watu wawili kifungo cha miaka miwili jela kwa kosa la kula njama ya kumuua Rozalia Kema.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Jaji wa Mahakama hiyo, Peter Dyansobera, baada ya washtakiwa kukiri kosa la kula njama ya kutaka kufanya mauaji hayo.

Washtakiwa waliohukumiwa kifungo hicho ni Samuel Kazimili (36) na Emmanuel Magesa (28), wote wakazi wa Kijiji cha Isima, wilayani Geita.

Kazimili na Magesa walipandishwa kizimbani jana mbele ya Jaji Peter Dyansobera na waliposomewa shtaka lao walikiri kuhusika na kosa hilo.

Katika kesi hiyo, upande wa mashtaka, uliongozwa na Wakili wa Serikali Winfrida Mpiwa na upande wa utetezi, ulikuwa ukiongozwa na Wakili wa Kujitegemea Paulo Michael ambaye alikuwa akiwatetea washtakiwa wote wawili.

Jaji Dyansobera alisema baada ya washtakiwa wote kukiri kosa lao, alimwambia Wakili wa Serikali kuwasomea maelezo ya awali.

Akisoma maelezo ya awali, Wakili Mpiwa alidai kuwa tarehe isiyofahamika, Februari mwaka 2016, washtakiwa kwa pamoja walikula njama ya kumuua Kema kwa malipo ya Sh. 900,000.

Alidai kuwa baada ya kufanya makubaliano hayo, washtakiwa hao waliondoka hadi Kijiji cha Isima nyumbani kwa Kema na kumweleza kuwa: "Tumekuja hapa kwako kwa lengo la kukuua na tumepewa fedha Sh. 900,000 ili tukuue. Lakini ukitaka tusikuue na kunusuru maisha yako, inatakiwa utupatie Sh. milioni mbili ili tusikuue."

Mpiwa alidai kuwa baada ya Kema kupewa taarifa hizo, aliwaambia washtakiwa kuwa: "Kwa sasa sina hizo fedha, lakini Febuari 15 mje hapa nyumbani niwapatie fedha hizo."

Alidai kuwa baada ya kuambiwa hivyo, washtakiwa hao walikubaliana na ombi hilo kisha kuondoka.

Baada ya washtakiwa hao kuondoka, alidai kuwa Kema alikwenda kwenye Ofisi ya Kijiji cha Isima na kutoa taarifa kuhusiana na tukio hilo na ilipofika siku ya miadi, majira ya saa 9:00 mchana, washtakiwa hao walifika nyumbani kwa Kema ili kuchukuwa Sh. milioni mbili walizokuwa wameahidiwa.

Alidai kuwa baada ya washtakiwa hao kufika nyumbani Kema, alipiga kelele (kwa Kisukuma mwano) na watu walikusanyika kwa kushirikiana na mgambo wa kijiji hicho na kuwakamata washtakiwa na kuwapeleka katika ofisi ya kijiji. Baada ya hapo waliwapigia simu polisi ambao walifika na kuwachukua washtakiwa hadi Kituo cha Polisi Geita na walipohojiwa walikiri kula njama ya kumuua.

Wakili alidai baada ya mahojiano, washtakiwa wote kwa pamoja walipelekwa mahakamani ili sheria ichukue mkondo wake.

Baada ya Wakili Mpiwa kumaliza kuwasomea maelezo ya awali, Jaji Dyansobera aliwauliza washtakiwa kama maelezo hayo ni ya kweli ndipo walipojibu kuwa ndiyo.

Kutokana na washtakiwa kukiri kosa la kula njama ya kumuua Kema, Jaji Dyansobera alisema washtakiwa wanatiwa hatiani kwa kosa walilioshtakiwa nao na mahakama inawataka wajitetee ili iwapunguziwe adhabu.

Washtakiwa hao wakiongozwa na wakili wao, Mihael, waliomba mahakama iwapunguzie adhabu kwa kuwa wana familia zinawategemea na pia wamekaa mahabusu kwa muda wa miaka sita na siku 15.

Upande wa mashtaka ukiongozwa na Wakili Mpiwa uliomba mahakama hiyo itoe adhabu kwa mujibu wa sheria.

Jaji Dyansobera alitupilia mbali utetezi huo na kusema katika dunia hii mtu akiwa na familia anatakiwa utende mema ili kuhudumia familia yake.

"Hawa washtakiwa bado ni vijana, mtu anatakiwa avune kile alichopanda, washtakiwa wote kwa pamoja mtatumikia kifungo cha miaka miwili jela kila mmoja na upande ambao haujaridhika na uamuzi huu rufani iko wazi," alisema Jaji.



Baadhi ya wakazi wa Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani, wakiwa wamebeba vyakula pamoja na mafuta ya kupikia, vilivyotolewa na Taasisi ya Afrika Relief Organizational kwa kushirikina na Taasisi ya Rahma International Society za nchini Kuwait katika kuadhimisha Siku ya Uhuru wa Taifa hilo, wilayani humo, hivi karibuni. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Ridhiwani: Mabaraza ardhi yajikite kusuluhisha

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Ridhiwani Kikwete, ameyaelekeza mabaraza ya ardhi kujikita kwenye kutoa usuluhishi badala ya uamuzi ili kupunguza migogoro kwenye maeneo yao.

Ridhiwani ambaye ni Mbunge wa Chalinze alitoa maelekezo hayo jana alipokuwa akizungumza na wakazi wa vijiji vya Kwaikonje, Masimbani na Miono katika ziara yake ya kusikiliza kero za wananchi.

"Mabaraza ya ardhi msiende mkafanya kazi ya kuamua juu ya nani ana haki nani hana katika ngazi ya kijiji na kata, jukumu lenu ni kupatanisha, kuamua kwa busara," alisema.

Alisema mabaraza ya ardhi ya vijiji na kata kwa mujibu wa sheria ni mabaraza ya usuluhishi na upatanishi, na kwamba wenyeviti wa mabaraza hayo wanatakiwa kujikita katika nafasi zao za kuwa wenyeviti wa vikao vya usuluhishi na si kutoa uamuzi.

"Nimekutana na rundo la malalamiko ndani ya ofisi yangu, mabaraza yetu ya ardhi mara nyingi hayaonekani kutenda haki katika maeneo yetu na watu wengi wanayalalamikia, hilo ni kwa upande mmoja upande wa pili wasimamizi wa sheria hatutoi tafsiri ya sheria yanatakiwa kufanya nini," alisema.

"Mabaraza ya maamuzi ni kwa ngazi ya kuanzia wilaya kwenda juu tunahitaji kufanya kazi kubwa kumaliza migogori ya ardhi," alisisitiza Ridhiwani.

Alisema kunahitajika kufanya semina na kupeana elimu ya mabadiliko ya sheria na namna mabaraza yanavyotakiwa kufanya kazi ili kuondoa kasi ya migogoro ya ardhi.

Akizungumzia kuhusiana na kero nyingine za wananchi, Ridhiwani alisema atahakikisha taasisi za serikali zinapatiwa huduma ya umeme, lakini utatuzi wa vikwazo katika Kituo cha Afya Miono vinafanyika kwa haraka.

Diwani wa Miono, Juma Mpwimbwi, alimwomba Ridhiwani kutafuta namna ya kumaliza migogoro hiyo kwani wapo wananchi wamevuka mipaka na kuvamia hifadhi ya kijiji, hivyo kusambabisha migogoro kuendelea.

Mpwimbwi pia alimwomba kusaidia upatikanaji wa watumishi katika Kituo cha Afya cha Miono kwani waliopo hawatoshelezi mahitaji ya wananch na pia upatikanaji wa jengo la upasuaji kituoni hapo.

Baadhi ya wakazi wa Miono walisema ni vema timu ya wataalamu kutoka Wizara ya Ardhi ikafuatilia suala la migogoro ili wananchi waweze kufanya shughuli nyingine za maendeleo badala ya kupambana na kero hizo mara kwa mara.

**HABARI KITAIFA**

# Mwanafunzi chekechea ajeruhiwa, auawa na fisi wakati akiuza nyanya

**Na Jumbe Ismailly, SINGIDA**

MWANAFUNZI wa darasa la awali katika Shule ya Msingi Mtoa, Iramba mkoani Singida, Neema Isaya (7), amefariki dunia wakati akipatiwa matibabu katika zahanati ya kijiji cha Mtoa baada ya kujeruhiwa na fisi.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Singida, Kamishna Msaidizi (ACP) Stella Rutabihirwa, alithibitisha hayo jana alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari kwamba tukio hilo lilitokea Februari 27, mwaka huu, saa 11:45 jioni katika kitongoji cha Mpambaa, kijiji cha Mtoa. Alisema mtoto huyo alijeruhiwa na fisi akiwa na dada yake, Eliwaza Isaya (10) ambaye ni mwanafunzi wa darasa la tatu katika shule hiyo.

Ruhahibirwa alisema siku ya tukio, mwanafunzi huyo akiwa anauza nyanya za nyumbani kwao, wakiwa wanapita katikati ya shamba la mahindi, ghafla walishambuliwa na fisi ambaye alimshambulia kichwani na kumsababishia majeraha makubwa.

Alisema polisi kwa kushirikiana na askari wa Kikosi cha KDU pamoja na polisi kata, walifanikiwa kumuua fisi huyo baada ya Neema kupiga yowe na wananchi kufika katika eneo hilo.

Katika hatua nyingine, watu wanane wanashikiliwa na polisi mkoani Singida kwa tuhuma za wizi wa vitu mbalimbali yakiwamo makasha 50 ya dawa za binadamu aina ya Artemether+ Lumifatrine/ALU mali ya serikali na pikipiki tano aina ya Sanlg na Haujue.

Kamanda Rutahibirwa alisema makasha hayo ya dawa yaliyokamatwa, yaliibwa katika Hospitali ya Wilaya ya Manyoni na kwamba watuhumiwa watatu walikamatwa wakati wengine sita, wote wanaume, walikamatwa kwa tuhuma za wizi wa pikipiki.



Mtaalamu wa Ununuzi wa Benki ya Dunia ambaye ni Mratibu wa nchi za Tanzania, Malawi, Zambia na Zimbabwe, Ishtiak Siddique, akipeana mkono na Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Kusimamia Ununuzi wa Umma (PPRA), Dk. Irene Isaka, alipotembelea ofisi za makao makuu ya mamlaka hiyo akiwa na ujumbe wa Benki ya Dunia, hivi karibuni. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wanaharakati waomba uwapo usawa kijinsia mgawanyo majukumu

**Na Yasmine Protace**

WANAHARAKATI wametaka uwapo usawa wa kijinsia katika mgawanyo wa majukumu, ikiwamo ndani ya vyama vya siasa.

Pendekezo hilo limetolewa ikiwa ni kuelekea Siku ya Wanawake Duniani, ambayo hufanyika kila Machi 8.

Hayo yalisemwa na washiriki wa semina za jinsia na maendeleo (GDSS), ambazo huratibiwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP).

Hawa Juma, mshiriki wa GDSS, alisema kuwa usawa unatakiwa kuwapo katika mgawanyo wa majukumu ya kila siku.

"Tunapoelekea Siku ya Mwanamke Duniani, tunataka usawa wa kijinsia katika majukumu uwepo, kwa sasa ukiangalia katika baadhi ya vyama vya siasa viongozi wote wa ngazi za juu ni wanaume," alisema.

Aliongeza kuwa kuwapo kwa viongozi wa juu wanaume pekee kunasababisha mgawanyo wa majukumu usiangalie jinsia zote mbili na majukumu yatakuwa yamemlenga moja kwa moja mwanaume pekee.

Aliongeza kuwa uwepo utaratibu ambao utavibana vyama vyote ambavyo katiba zao zitaonyesha kuwabeba wanaume pekee.

Hassan Hamza alisema katika kuelekea Siku ya Mwanamke Duniani, vyama viwe na sera mpya yenye usawa katika vyama vya siasa kati ya mwanamke na mwanaume. Tatu Ally alisema ni wakati wa wanawake kujitokeza kugombea nafasi zozote katika uongozi na sio kurudi nyuma.

Aliongeza kuwa wanawake wana uwezo wa kuongoza na wakaleta mabadiliko makubwa ya uongozi katika kitengo ambacho watakuwapo.

# Elimu saikolojia yasisitizwa kwa vijana wenye msongo mawazo

**Na Francis Godwin, IRINGA**

ELIMU ya saikolojia inahitajika kwa vijana chini ya miaka 25 wanaotoka katika mazingira magumu ili kukabiliana na msongo wa mawazo na sonona, imeelezwa.

Mwenyekiti wa Chama cha Watoa Huduma za Kisaikolojia Tanzania, Dk. Heriel Mfangavo, aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo kwa vijana kutoka kata za Mdabulo, Ihanu na Luhunga, Mufindi mkoani Iringa.

Alisema vijana hao ni wadogo, hivyo kama hawatapatiwa tiba ya kisaikolojia mapema, tatizo hilo linaweza kukua zaidi ukubwani na kujiingiza katika matukio ya hatari yakiwamo mauaji au kujiua.

"Mfani ni mabinti waliopata mimba utotoni kwa kubakwa au kurubuniwa. Hali hiyo huwa haifutiki kirahisi kwenye akili zao, hivyo lazima elimu ya kisaikolojia wapatiwe mapema ili wasiendelee kuteseka au kutesa watoto," alisema.

Pia alisema vijana walionyanyasika kwenye familia kwa kutelekezwa na baba mzazi wakiwa wadogo au kupokonywa mali huwa wanakuwa na visasi hadi ukubwani.

Kundi lingine, alisema ni la watu wenye ulemavu ambao baadhi yao wanaishi na msongo wa mawazo na sonona kutokana na hali waliyo nayo huku akibainisha kwamba suala la ulemavu linasababisha watu wengi kuishi na msongo wa mawazo na hata kupata matatizo mengine ya kiakili.

Alisema wanasihi watakaofanya kazi katika mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM) wanatakiwa kubaini vitu vinavyosababisha msongo wa mawazo katika jamii ya watu wenye ulemavu na kuvitafutia ufumbuzi.

Kutokana na ukubwa wa tatizo kwa vijana hao na watu wenye ulamavu, alisema mafunzo hayo yatakuwa na faida kubwa kwao na kuondokana na utegemezi.

Dk. Mfangavo alisema mradi huo wa YAM ni mkombozi mkubwa kwa jamii ya wana Mufindi hasa maeneo ambayo yanazungukwa na mradi huo kwa kuwa utasaidia jamii yenye uhitaji kuishi kwa furaha zaidi.

Aliyataja baadhi ya mambo yanayosababisha msongo wa mawazo na sonona kuwa ni kukataliwa, kutengwa na unanyapaa wa kiuhusiano.

Pia alisema hali duni ya kiuchumi husababisha watu kupata msongo wa mawazo, hivyo kupitia mafunzo hayo yanayotolewa ni wazi jamii itapunguza tatizo la msongo wa mawazo na hata kufanya shughuli kwa ufanisi zaidi.

Baadhi ya vijana wanaotoka katika familia duni, waliokatisha masomo kutokana na changamoto mbalimbali zikiwamo mimba kwa mabinti, walipongeza mradi wa Youth Agency Mufindi (YAM) kwa kuwafikia na kuwapa mafunzo ya afya ya akili na msaada wa kisaikolojia.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo, Felix Kitinusa na Diana Ngongomi, walisema elimu hiyo ni fursa kubwa kwao kwa kuwa kupitia mafunzo hayo, ni mwanzo kwao kujitambua na pindi watakapojitambua ni rahisi kufanya shughuli za kiuchumi.

"Tunaamini kupitia mafunzo haya tumepata ukombozi katika maisha yetu na familia tunazotoka maana bila kujitambua ni vigumu kubaini nini cha kufanya," walisema na kubainisha kuwa wana matarajio ya kupewa nguvu ya uwezeshwaji ili kutimiza ndoto zao kimaisha.




Watanzania tuachane na uheshimiwa, turudie udugu



## SIDO ilivyowaunga wajasiriamali Morogoro kupitia kongano bidhaa

Ukurasa 14

BUFE
IJUMAA MACHI 4, 2022
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI...

**KUTANA NA DOMINA HUGO**

# Shujaa aliyetumikia jiko kuu Ikulu, sasa anawanoa wa shahada upishi

- Aanika kujiamini kulivyompa majibu
- Msimamo wake umebaki kuwa nguzo

**Na Christina Mwakangale**

UKIMUONA ni mtu mzima kiumri, ila akibaki katika hadhi yake kuwa mwanamama anayependeza hasa wakati wote.

Pia, ukirejea methali 'utu uzima dawa', uzoefu wake katika fani sasa ukitimu leo miaka 30 na ushee, sasa anashika chaki kurejesha ujuzi wake kwa wataaluma wajao kuwafunza mapishi na yanayoendana nayo. Ukimsikia, unaweza kukimbia kama si kubaki kinywa wazi!.

Huyo ni Mama Domina Hugo, ambaye pamoja na yote, ameshashiriki vilivyo katika heshima ya kukata vitunguu katika jiko la Ikulu kwa uongozi wa vipindi viwili tofauti na kupata daraja lote la hadhi njema.

Ndani ya falsafa 'kinamama wakiwezeshwa wanaweza' anasema ameshakuwa jasiri Ikulu kutenda ambalo baadhi ya wenzake katika timu ya wasaidizi walihofu, akalimaliza na kupewa baraka na mkuu husika 'hakuna shida.'

Hapo anafafanua: "Pamoja na kazi ya uhudumu katika hoteli jamii kutafsiri kwa namna tofauti, kwamba ina maadili mabaya, nami nilipowaambia familia yangu napenda kazi hii, baadhi walikasirishwa, ila misimamo yangu na kuzingatia kazi imenifanya nifike hapa."

Mama Domina anaendelea: "Kufanya kazi vizuri kwa nidhamu kulinifanya nifanye kazi Ikulu, kama 'House Keeper' kwa kipindi cha Rais (Bejamin) Mkapa na (Jakaya )Kikwete. Hapo nilihudumia pia wageni waliofika wakiwamo marais wa Afrika na Afrika Mashariki, (Olusegun) Obasanjo, (Yoweri) Museveni, (Mwai ) Kibaki.'

Mbali na utumishi huo, pia anakumbusha kujivunia hali ya ujasiri, nidhamu na ukweli wake katika nafasi ya jinsia yake kama mwanamke. Anasimulia: "Nimehudumu 'two presidency' (vipindi viwili vya urais). Siku moja ninayoikumbuka tulikuwa tumepewa kazi (kumhudumia rais).

"Halafu venue (eneo) likawa limebadilishwa, ghafla siku hiyo. Kufika pale ilitakiwa 'ni- save' (kuhudimia) chakula saa saba. Kwa kuwa 'venue' ilibadilishwa, chakula kikachelewa kidogo, nyama haijaiva.

"Muda kidogo tu Rais (hakumtaja) anafika...nikamwambia 'mheshimiwa samahani chakula kitachelewa kidogo naomba muda wako'...Nakumbuka kile alichoniambia alisema 'mama chukua muda wako'. Confidence, confidence (kujiamini) usiharibu kazi, lakini confidence."




Mama Domina Hugo. **PICHA: CHRISTINA MWAKANGALE.**

**ALIKO SASA**

Kwa sasa Domina ni Mkufunzi anawanoa wanaosoma kwenye ngazi tofauti kati ya stashahada na shahada katika Chuo cha Taifa cha Utalii.

Rai yake anawaasa wanafunzi wake, kwamba wasiishie matarajio ya kuajiriwa pekee, pia wafikirie kujiajiri, ndani yake wakitafakari ushindani uliopo sokoni wa kuziwania fursa za ajira ni mkubwa.

Katika hilo anawahimiza wanafunzi cha muhimu kuwa wabunifu, wanajituma, wawekaji nia na kufikiri zaidi, kwamba ni mambo yatakayowaletea nafuu.

Domina anawapa mbinu wanafunzi kwamba: "Bidii yangu tangu nikiwa masomoni ilinifanya nifahamike na kila mmoja kutokana na kujituma. Nilipata ufadhili wa masomo Kenya Utalii College, nikisomea fani ya 'House Keeping' ngazi ya cheti mwaka 1990 hadi 1992."Nilipohitimu nikachukuliwa na ILO (Shirika la Kazi Duniani) na UNDP (Mpango wa Maendeleo wa Umoja wa Mataifa)..."

Anakumbusha kwamba alishafundisha katika Chuo Cha Utalii Maruhubi Zanzibar, kati ya mwaka 1992 hadi 1994.

"Kazi niliwahi kufanya Embassy Hotel (Dar es Salaam) mwaka 1988 wakati nipo hapa Dar es Salaam. Nilifanya vizuri mwaka mmoja tu hadi nikapata ufadhili wa masomo zaidi," anasimulia

Ni wazo la Mama Domina, ambalo alitoa katika mahafali ya Chuo cha Utalii, na iliyoungwa mkono na mwanama, Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Mary Masanja akiwaasa : "Chagua moja kuajiriwa, au kujiajiri, usiende kuwa mzigo kule uendako. Mkawe wabunifu. Kwa miaka 60 ya Uhuru, hatujawahi kuwa na vazi rasmi, muwe wabunifu wa vazi hili ili kuitangaza Tanzania."

BIASHARA

KUELEKEA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI...

# Wanawake visiwani wanavyopambana na zao mwani linalopitia 'milima na mabonde'

- Walimaji wakuu, mtihani wao soko na tabianchi
- Umoja wa Mataifa Zanzibar nao wawafuatilia

**Na Rahma Suleiman, Unguja**

KILA ifikapo Machi 8 ya kila mwaka, dunia inaadhimisha Siku ya Wanawake Duniani na Tanzania ikiwa sehemu yake, imo katika maadhimisho hayo. Panapo majaliwa, kilele kinachokusanya na kupaza vigelegele vya kinamama ni Jumanne ijayo au siku nne zijazo.

Kama ilivyotambulishwa kaulimbiu iliyoko mwaka huu ni "Zingatia usawa wa kijinsia kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa maisha endelevu".

Kimsingi, athari za mabadiliko ya tabianchi zinajulikana, kwamba huathiri shughuli za kibinadamu, hali ya hewa na maafa yanayotokea kwa jamii.

Duniani kote wanawake wanaathirika zaidi kutokana na umaskini, kutokuwa na uwezo mkubwa zaidi ya wanaume kiuchumi, hivyo inawaangukia hali inayowafanya washindwe kujikwamua kutoka katika majanga yanayoharibu miundombinu yao ikiwamo katika ajira.

Uchumi wa Zanzibar, nao unategemea sana tabianchi na sehemu kubwa ya pato la taifa, ajira na maisha yao yanahusiana na shughuli zinazotokana na tabianchi, katika mazingira ya pwani, kilimo na utalii.

Ongezeko la joto, mvua zisizotabirika, upepo mkali na kupanda kina cha maji ya bahari, ni miongoni wa athari za mabadiliko ya tabianchi.



Namna ulivyo uzalishaji wa zao la mwani katika ukanda wa bahari, visiwani Unguja. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

**YANAYOJIRI SHAMBANI**

Kuongezeka joto baharini, nako kunatajwa kuathiri kilimo cha mwani Zanzibar, ambacho asilimia 90 ya kilimo hicho kinalimwa na wanawake.

Mwanaisha Simai Makame ni mkazi wa kijiji cha Paje Kusini Unguja. Ni miongoni mwa wanawake wanaolima zao la mwani, akisema hivi sasa uzalishaji wake uko katika sura ya kubahatisha, hata kuna wakati unapita mwezi mzima bila ya kuguswa, kutokana na mabadiliko ya hali ya hewa.

"Jua limekuwa likiathiri sana kilimo chetu. Hivyo unakuta miezi miwili tunalima na mwezi mzima tunashindwa kulima, kwa sababu kila tukipanda mwani wakati wa jua mwani unaungua," anaeleza.

Mwanaisha, ambaye ni Mwenyekiti wa Kikundi cha Furahia Wanawake, wanaojishughulisha na ulimaji mwani, anasema kwa sasa wanaotesha mbegu inayoitwa 'Sea weed', wakiacha aina ya zamani kwa sababu ya mabadiliko ya tabianchi.

"Kikundi chetu kilianza tokea mwaka 1990, lakini mwaka 2019 ndio tukaanza kuunda ushirika na asilimia kubwa ya wanachama wake ni wanawake. Kazi yetu tunalima mwani, kwa kutengeneza bidhaa mbalimbali ikiwamo sabuni," anasema.

Anafafanua mwanzo ushirika huo ulikuwa wa kinamama zaidi ya 50, lakini kutokana na kilimo hicho kukabiliwa na changamoto ikiwamo mabadiliko ya tabianchi, yameshusha uzalishaji mwani, pia bei ndogo na wakulima wengi wamekata tamaa kuachana na kilimo hicho, sasa wamebaki 34.

Mwanaisha anafafanua kuwa, miongoni mwa mafanikio waliyopata ni kuongeza bei ya mwani kutoka Sh.150 kwa kilo hadi hadi Sh. 500, hata kuchangia nyongeza ya kipato cha kujikimu kimaisha, ikiwamo cha kusomesha watoto, anatoa rai wadau wawasaidie kupata vifaa vya kuendeleza kilimo chao.

Fatma Jabu, yuko katika kinamama walioachana na kilimo cha mwani, naye analalamika akitolea ufafanuzi uamuzi wake kwamba kilimo hicho sasa kina gharama kubwa na faida ndogo, hata imemlazimu kuachana nacho, akihamia biashara nyinginezo.

"Kilimo cha Mwani kina kazi kubwa, kwanza vifaa vyake ni bei, soko hafifu, pia kinahitaji uwe na nguvu na afya nzuri, kwa sababu kilimo hiki kinalimwa baharini na kutokana na mabadiliko ya tabianchi, hivi sasa ni lazima kipandwe katika kina kirefu cha maji ya bahari," anaeleza.

Hata hivyo, hadi sasa bado Zanzibar inatajwa kuwa nchi ya tatu duniani kuzalisha kwa wingi na ubora.

**WATAALAMU WA MWANI**

Wataalamu wa sayansi ya bahari wakiendelea na utafiti, pia wanajaribu kutafuta mbinu mbalimbali za kukomboa kilimo hicho.

Dk. Narman Jidawi, ni mtaalamu wa mazao ya baharini, anasema kilimo cha mwani kikisuasua kitawaathiri sana wanawake na ndio maana wameanza kutafuta mbadala wa kuwafaidisha wakulima kupitia mbinu mpya za kulima katika maji mengi ya baharini.

Flower Msuya, ni mtafiti wa zao la mwani kutoka Chuo cha Sayansi ya Bahari Dar es Salaam, anasema kilimo chake bado kina soko kubwa Zanzibar. Anasema mwani ni zao la pili kuingizia Zanzibar fedha za kigeni na kilimo chake kinawanufaisha zaidi wanawake visiwani humo.



"Katika utafiti wetu tumebaini kuwa mwani unaoitwa 'cottonie' unaweza kulimwa kwenye maji mengi na ndio mwani bora zaidi hivyo tunatumia (tuber note) kulima mwani huo, njia hiyo inatumia neti na bomba kupanda mwani kwenye bahari badala ya vijiti," Flower anafafanua.

Anaeleza, baada ya kulima mwani katika maji ya kina kifupi, ikabadilishwa na kulimwa kwenye kina kirefu na teknolojia hiyo tayari wameshaanza kuitoa kwa walima mwani, ila changamoto iliyopo ni shida ya vifaa.

"Wanawake wanaolima mwani hivi sasa, wanajifunza kuogelea ili waweze kulima mwani katika maji mengi bila changamoto," anasema Mtafiti Flower.

**UCHUMI WA BLUU VS KIJINSIA**

Mwenyekiti wa Taasisi ya Maisha Bora, Mama Mariam Mwinyi, anasema kuna uwezekano mkubwa wanawake kustawi katika Uchumi wa Bluu, ikiwa sehemu ya usawa wa kijinsia, utakaoboreshwa na kuunganishwa katika maeneo yote. ikiwamo kilimo cha mwani.

Anasema kunahitajika mabadiliko ya kisera na kifikra, ili vikwazo vinavyozuia uwezeshaji wanawake kiuchumi katika sekta ya uchumi wa bluu, ikiwamo sheria zinazomlinda mwanamke.

Mariam anasema, wakati Zanzibar inatekeleza sera yake ya Uchumi wa Bluu, ni lazima kuhakikishwe wanawake wanainuliwa kiuchumi na hawaachwi nyuma.

Anaeleza, ili kukabiliana na changamoto hizo, sera, mikakati na hatua zinatakiwa kushughulikia mahitaji mahususi ya wanawake na wasichana na wakawezeshwa kutambua haki zao kiuchumi.

Anatoa takwimu kuwa asilimia 32 ya kaya zinazoongozwa na wanawake Zanzibar, zinafanya kazi katika sekta za kilimo au uvuvi, na wao ndio wengi katika sekta ya utalii na ufugaji samaki, hivyo ni muhimu wakawezeshwa katika uchumi wa bluu.

**KINA MAMA WA UN**

Mwakilishi wa Asasi ya Wanawake ya Umoja wa Mataifa (UN Women), Hodan Addou, anaeleza mchango wa wanawake ni mkubwa katika mapato ya kaya na usalama wa chakula na kiuchumi, lakini bado kazi zao katika uvuvi zinakosa kutambuliwa rasmi na wanawake hawajawakilishwa sana katika sera na kufanya maamuzi.

Anafafanua kuwa huduma za bahari zinajumuisha zaidi ya asilimia 37 ya Pato la Taifa, hivyo wanatakiwa katika ngazi za kuamua.

Pia, anataja mabadiliko ya kijinsia katika Uchumi wa Bluu Zanzibar yanawezekana na UN Women bado inajitolea kushirikiana na washirika kulinda maslahi na haki za wanawake ndani ya sekta hiyo ya Uchumi wa Bluu.

**JUHUDI ZA SERIKALI**

Akizungumza na uongozi wa Benki ya AFREXIM, Rais wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi, ameomba kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ), katika kupata mchanganuo wa masoko wa zao la mwani, ili wakulima wake wanufaike.

Anasema Zanzibar inategemea mazao makuu mawili ya biashara, karafuu na mwani ambayo wakulima wake wanakabiliwa na changamoto kubwa ya bei ya mauzo iko chini zaidi.

"Ni eneo ambalo tunahitaji kupata ushirikiano ili kuliongezea thamani zao hilo pamoja na kuinua kiwango cha bei ili wakulima wetu waweze kunufaika," anasema Rais Mwinyi.

SMZ pamoja na kuegemea utalii kuwa chanzo chake kikubwa cha mapato, pia zao la mwani kwa sasa linapewa kipaumbele baada ya zao mweza wake - karafuu, kupoteza bei katika soko la dunia.

Kwa mujibu wa bajeti iliyopita ya Zanzibar ya mwaka 2022/2023, kwa muda wa miezi tisa kutoka Januari hadi Septemba mwaka 2021, Zanzibar ilisafirisha tani 8,470 za mwani zenye thamani ya Sh. Bilioni 8.1

Kwa upande wa zao la karafuu, zilisafirishwa tani 5,308.13 zenye thamani ya Shilingi bilioni 90.7.

TAFAKURI YA MLALAHOI

# Watanzania tuachane na uheshimiwa, turudie udugu






**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: jkulangwa@yahoo.com

JUZI kati hapa kama kawaida yangu, nikawa kijiweni kusogoa na wana nzengo wenzangu, mara likaja gari fulani la kifahari, likaegesha mbele yetu na akashuka mwanadada hivi mlimbwende.

Akatusalimia kwa heshima tu, kumbe anafahamiana na mwenzetu pale, akatutambulisha kuwa ni ndugu yake na alikuwa anapita akatuona, hivyo akaona vema atusabahi kwa kuwa anatoka mkoani.

Tukafurahi, tukamkaribisha kijiweni kwa sababu alionekana kuwa mcheshi na anayeweza kuzoea mazingira haraka, huku pia akipenda mzaha na utani, hata masihara.

Dada yetu tukamzoea, mara tukaingia kwenye mazungumzo ya kina kuhusu masuala ya kisiasa na kiuchumi, naye ghafla akasema alipokuwa hajawa 'mheshimiwa' hakuwa anafahamika kama ilivyo sasa.

Tukazungumza mengi sana kuhusu nchi yetu na ikaonekana anaijua fika na hata siasa zake anazijua, ingawa kuna nyakati alikuwa mwamba ngoma, akivutia sana ngozi upande wake na wa chama chake.

Hilo mimi halikunizingua sana, kwa sababu chama chake nami ni changu, ingawa kuna nyakati kinafanya madudu nami huwa simezei, ninapoona hivyo huwa sisiti kukibabua na kukizingua vilevile.

Kilichonigusa ni ile ya kusema "nilipokuwa sijawa mheshimiwa" nikawaza sana hili neno mheshimiwa lina maana gani katika jamii, ingawa katika utambulisho tuliambiwa dada ni mbunge wa hivi viti hivi.

Kwa hiyo, nikaelewa kuwa alimaanisha kuwa wakati hajawa mbunge hakuwa akifahamika na sasa ni mbunge anafahamika na tena mheshimiwa, ndiyo kabisaa! Kwamba ni tofauti sana na sisi kajamba nani.

Nikajiuliza hivi uheshimiwa hupatiwa mafunzo au inakuwaje? Polisi angesema wakati sijawa askari, au mwalimu angesema wakati sijawa mwalimu, daktari na mwanasheria hivyo hivyo, kwa sababu ni taaluma.

Hivi ubunge ni taaluma? Hivi udiwani ni taaluma? Sijajua kuhusu uhakimu na ujaji kwa sababu hao mimi huwajua kama wanasheria wasomi, lakini wanazidiana ngazi, kuanzia mawakili, mahakimu na majaji, nadhani sina uhakika vizuri hapo. Taaluma hapo ni sheria bila shaka.

Turudi kwa dada yetu huyu anayewakilisha watu wengi, kusema hivyo kwa kweli kulinifanya nikamkumbuka Hayati Baba wa Taifa, Mwalimu Julius Nyerere, ambaye kuna wakati akasema; kuanzia sasa tuitane ndugu!

Rais akawa ndugu mpaka mwanafunzi wa darasa la kwanza akawa ndugu, Watanzania tukiitana ndugu na kwa kweli ilisaidia sana kuondoa dharau katika jamii. Kila mtu akawa ndugu wa mwingine.

Leo wapo wateule wetu wanaotaka waitwe waheshimiwa, mpaka mtu anasema kabla sijawa mheshimiwa, yaani sawa kabisa na daktari anayesema kabla sijamaliza masomo yangu na kuhitimu kuwa daktari!

Hivi tukijiuliza Bunge la ndugu mbunge, ndugu Spika, ndugu Naibu Spika, ndugu Waziri na ndugu Naibu Waziri na la mheshimiwa mbunge, mheshimiwa Spika, mheshimiwa Naibu Spika na mheshimiwa Waziri, tofauti yake ni nini?

Nadhani hata katiba yetu, inasema kila mtu anastahili kuheshimiwa. Tunapoheshimiana muda wote iwe mbele ya sheria au ndani ya katiba, ndipo tunapoweza kujitapa kuwa tu wamoja na wenye mshikamano na tunaweza kusukuma gurudumu la maendeleo bila kujibagua kuwa huyu matawi ya juu huyu mzizi wa chini.

Kwa kweli huku tunakokuona hivi sasa, inatuchanganya kidogo sisi hasa katika taifa hili ambalo mimi huliona kuwa teule miongoni mwa mataifa, ambalo limekuwa na amani miaka nenda rudi ya kuwa mfano.

Mwalimu Nyerere alituachia taifa lenye umoja, lenye kuheshimiana, kushikamana na amani isiyotetereka. Daima tusigawanywe na hatimaye tusisambaratishwe kwa mambo madogo kama haya.

Tutambue tu kuwa mheshimiwa ni kila Mtanzania. Napendekeza, turudi tulikokuwa, tuitane na kutambulishana kama ndugu, na si vinginevyo. Kwishney! Alamsiki!

BIASHARA

# SIDO ilivyowaunga wajasiriamali Morogoro kupitia kongano bidhaa

## • Waneemeka kibiashara, bila mikopo mikubwa

**Na Christina Haule, Morogoro**



Kaimu Meneja wa SIDO Mkoa Morogoro, Joan Nangawe, akiangalia utendaji kazi wa karakana ndogo ya MECI, wakati mafundi wakitengeneza beseni la kuokea mikate.

WAJASIRIAMALI mkoani Morogoro wako katika ngazi wanashauriwa kujiunga na kongano la bidhaa lilioanzishwa na Shirika la Kuhudumia Viwanda vidogo (SIDO), ili kunufaika na shughuli zao, ikijumuisha mitaji waliyo nayo, badala ya kukimbilia kuendeleza biashara waliyo nayo.

Katibu wa Kongano la Chuma Morogoro (MECI), Omari Komba, ana ainisha mafanikio kwamba, kabla ya kuunganishwa kwenye kongano na SIDO, alikuwa na mtaji mdogo wa Sh. 300,000, ndipo akaamua kuomba mkopo SIDO.

Anaeleza kabla ya kupewa mkopo, akapatiwa mafunzo hata akabaini kutambua kuwa na mtaji zaidi ya Sh. Mil 20 zinazotokana na fedha mkononi na vitendea kazi hata akaachana na kukopa .

Komba anasema, alikuwa na mfumo wa kukopa benki na alipojiunga SIDO, ndipo alikokopa, nako baada ya elimu ameacha kukopa zaidi ya miaka minane sasa.

"Baada ya mafunzo nimebaini kuwa, kwa sisi ukikopa pesa kwenye uzalishaji inasumbua mno, sababu bidhaa zetu hazitoki papo kwa hapo.

"Mfano nikikopeshwa shilingi elfu 50 nitengeneze jiko ni hatua, niulize ni hatua, nitapata hela kweli hapo?. Ni heri kuchukua bidhaa kwa muuzaji, kwani hakuna riba ni marejesho ya nilichochukua tu," anafafanua na kuwaasa wajasiriamali wajiunge kunufaika na ubunifu huo wa SIDO.

"Wao wanajua, wakishaona hapa kunayumba wanajua pale kuna somo gani tupeleke. Mfano, juzi walileta somo la wachomeleaji na fundi mtaalamu kwa kuboresha bidhaa zetu, tukapata mafunzo ya bure ya wiki," anasema.

"Kwa sababu SIDO kwa hatua waliyo nayo, hawawezi kutafuta wajasiriamali mmoja mmoja mpaka mlangoni, bali wao wajasiriamali waone ujuzi kutoka kwa wenzao na kutamani kuutumia," anasema.

Anakumbuka binafsi alifanya kazi bila ya kuona faida na fedha aliyopata iliishia katika matumizi na familia, akisomesha watoto, sasa anajivunia hatua kuna mhitimu chuo kikuu, wengine wapo shuleni.

Komba anasema baada ya kuunganishwa kwenye kongano na SIDO mwaka 2008, anayo mabadiliko makubwa katika kazi, kwani mjumuiko wa mafundi wote uliopo unawafanya kuwa na ubunifu zaidi na nafasi pana.

"Kupitia kongano, mjumuiko wa mafundi wote tupo katika 'grade' (ngazi) zote na tunafanya kazi kwa kushirikiana, kwa kutumia viwanda vikubwa, vidogo, vya kati na vya chini kabisa, naweza kwenda popote na kutatuliwa shida yangu," anasema.

Komba anaeleza wameshapata misaada na mikopo ya mtu mmoja mmoja, vikiwamo vifaa na vitendea kazi akagharamia nauli pekee kuvitoa SIDO hadi kwenye maeneo yao ya kazi.

Anasema, kupitia kongano lao wamefanikiwa kupandisha mapato kutoka Sh. 294,500,000 mwaka 2005 hadi Sh. bilioni 1.4 mwaka 2017, huku ubora wa bidhaa wa kongano za vikundi 35 ukiongezeka.

Pia, anasema wameongeza uzalishaji na ununuzi wa teknolojia mpya.

**WAJUMBE NA YAO**

Mwana - kongano la Nguo Morogoro, Robert Joseph, anaishukuru SIDO kuwaunganisha mafundi wa nguo, hata wakaangukia mafanikio kitaifa, akisema kuna mafundi wengi wamekutana na kufahamiana na kuna mafundi wengi wanafanya kazi pamoja na kubadilishana uzoefu wa ushonaji nguo.

"Hivi sasa tunajuana, tunafanya kazi kama timu kwa pamoja kwa kushirikiana, sababu kile kitu ambacho nakiweza, mwingine hakiwezi. Akija kwangu, atajifunza bila ya malipo, tofauti na angeenda Dar es Saalam, angetoa gharama," anaeleza.

Anasema kupitia SIDO, wamefanikiwa kupata mashine kubwa ya kushona mitindo na kufanya kazi kwa muda mfupi, huku wakitoa nguo nyingi, pia kupata mafunzo ya juu kutoka ngazi ya juu.

Joseph anafafanua kupitia kongano, kwamba amewafundisha mafundi wachanga kutoka sita mwaka 2020 wakaongezeka hadi wanane mwaka jana, wakitoka mikoa ya Morogoro, Singida, Dodoma na Iringa kwa ada ya Sh. 30,000 kwa mwezi, wakiwa wameshaelewa.

**MENEJA SIDO**

Kaimu Meneja wa SIDO mkoa wa Morogoro, Joan Nangawe, anasema wao wanasimamia na kuhakikisha kazi wanazofanya zinakuwa endelevu na za kitaalamu, kuwafikia wengi mijini na vijijini, ikiwamo katika maendeleo ya teknolojia viwandani, masoko na uwekezaji, mafunzo, uendelezaji biashara na huduma za fedha.

Anafafanua kwamba wanawasaidia wajasiriamali kutambua teknolojia bunifu zinazotumika ndani na nje ya nchi, ikiwamo mifumo, mitambo na vifaa na wanavisambaza kwa wajasiriamali wakiwaelekeza namna ya kuvitumia.

Pia, meneja huyo anataja wajibu wao wa kuwafundisha masoko, sambamba na kuwaunganisha na Shirika la Viwango Tanzania (TBS) ili wapate nembo ya ubora, itakayowafungulia masoko kwa upana.

Lingine analolitaja, ni kuwafundisha namna bora ya kutumia Teknlojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ili wafanikiwe kupata masoko haraka.

Akizungumzia dhana ya Kongano, Nangawe anasema inawasaidia wajasiriamali kuwa sauti zao za pamoja na zinazosikika, hasa wanapokutwa na changamoto mbalimbali.

Nangawe anafafanua kuwa iwapo kila taasisi na mdau itaielewa dhana ya kongano na kuipa nafasi yake katika uzalishaji kwenye kazi, itawasaidia wajasiriamali kufaidika.

Anasema kuna kongano za aina 12 mkoani Morogoro yakiwemo yaliyoanzishwa mwaka 2006 na kutekeleza sera ya kuanzishwa na kuendeshwa viwanda, ili kuwawezesha wananchi na taifa lao kwa ujumla.

Hapo kuna orodha ya kongano kama za nyama, uhandisi, ushonaji nguo, usindikaji vyakula, kusaga nafaka, usindikaji mafuta alizeti, wafugaji kuku, utalii na sanaa, madini, useremala, pia bidhaa za mbao na chuma.

Hivyo, anaziomba taasisi za serikali, binafsi, mashirika ya kimataifa na watoa huduma mbalimbali kufanya juhudi za pamoja kuwafikia, wana- kongano na kusikiliza mahitaji yao ili wazalishe bidhaa, hata wawe na mchango katika kukuza uchumi wa Tanzania.

**HALI YA MIKOPO**

Kuhusu mikopo, Ofisa Usimamizi wa Fedha kutoka SIDO Morogoro, Allen Mhidze, anasema wametoa ushauri kwa wateja 389 wakiwamo watu binafsi na vikundi na wamewaunganisha wateja 17 na taasisi za fedha kupitia mfuko wa uwezeshaji kibenki (credit guarantee skim).

Anasema, katika kipindi cha mwaka 2020/21 wametoa mikopo yenye thamani ya shilingi milioni 315 kwa mikopo 142, ambayo kushuka kwa utoaji wa mikopo hiyo kumetokana na changamoto ya ugonjwa wa Uviko-19 na kwamba walilenga kutoa mikopo kwa wateja 408, wakiamini watafanikiwa kutoa mikopo zaidi.



Katibu wa Kongano la Nguo (KONGUMO), Robert Joseph (katikati), akimwonyesha Kaimu Meneja wa SIDO Mkoa wa Morogoro, Joan Nangawe, suti aliyoshona kwa ajili ya mteja wake. Kushoto kwake ni fundi anayejifunza akiendelea na kazi, kwenye ofisi iliyoko Kata ya Kihonda, mjini Morogoro. **PICHA ZOTE: CHRISTINA HAULE**



## HABARI DODOMA




Mkazi wa Kongwa, Tembo Makanyanga (kushoto), akimshawishi Jumamne Muna kumuuzia miguu ya ng'ombe maarufu kwa kutengenezea supu ya makongoro, eneo la soko la Kongwa, mkoani Dodoma jana. Mguu mmoja unauzwa kwa 4,000/-. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# TAKUKURU yaonya rushwa ya ngono sokoni

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Mkoa wa Dodoma, imeanza kampeni yake ya 'ulipo twaja' ikiwa ni mkakati wa kukabiliana na vitendo vya rushwa kwenye maeneo mbalimbali ikiwamo masoko, huku ikiwataka wanawake wafanyabiashara kutoshawishika kutoa rushwa ya ngono wanapohitaji maeneo ya biashara.

Akizungumza jana alipokuwa akitoa elimu ya rushwa ya ngono kwenye soko la Bonanza jijini hapa ikiwa ni kuelekea siku ya wanawake duniani ambayo hufanyika kila ifikapo Machi 8, Ofisa Mchunguzi Mkuu Kiongozi wa taasisi hiyo mkoani humo, Faustine Malecha, alisema kampeni hiyo imepanga kuwafikia asilimia 10 ya wakazi wa Dodoma ifikapo Machi 31, mwaka huu.

Alisema wanawake hawana sababu ya kutoa rushwa ya ngono kupatiwa maeneo hayo bali wanapaswa kufuata sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa kuyapata maeneo hayo.

Malecha alisema Kampeni hiyo imelenga kutoa elimu hiyo kwenye masoko, vijiwe vya bodaboda na maeneo mengine yenye mikusanyiko ili kukomesha vitendo hivyo.

"Elimu hii tuliyowapa ya rushwa ya ngono,tunaomba wazazi tusaidiane kuhakikisha inawafikia watoto waliopo shule za sekondari na vyuoni, wasisitizeni wasome na kuwajibika katika maeneo yao,"alisema Malecha.

Alisema wazazi wanapaswa kusaidiana na taasisi hiyo kutoa elimu ya rushwa ya ngono kwa watoto wao,kwa sababu suala la kupiga vita rushwa si la TAKUKURU peke yake,bali ni la watanzania wote. Naye, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Dodoma, Sosthenes Kibwengo alisema taasisi hiyo ina wajibu wa kuondoa vitendo vya rushwa nchini, ndio sababu ya kuanzisha kampeni hiyo ambayo inawafikia watu waliopo kwenye mikusanyiko wakiendelea na shughuli za ujenzi wa taifa.

Kibwengo alisema kuanzishwa kwa kampeni ya Ulipo Twaja walilenga kuwapata watu kulingana na aina ya kazi au biashara wanazofanya,ambao sio rahisi kuwapata kwenye mikutano mingine ya hadhara inayofanyika.

"Hii kampeni ni muhimu sana kwa sababu imesaidia kufikia idadi kubwa ya watu kutokana na kuwa inawafuata katika maeneo yao ya kazi kuwapa elimu huku wakiendelea na shughuli nyingine,"alisema Kibwengo.

Alisema Rais Samia Suluhu Hassan amesisitiza umuhimu wa kuzuia ubadhirifu wa mali za umma badala ya kusubiri zifujwe,hivyo TAKUKURU kutoa elimu ya rushwa kwa wananchi ili wasaidie kutoa taarifa pale wanapoona kuna mahali pana viashiria vya rushwa.

Alisema serikali inawekeza fedha nyingi katika miradi mbalimbali ya maendeleo, hivyo ni vema wananchi wakajua nini maana ya rushwa ili waisaidie taasisi hiyo kutoa taarifa kama kuna vitendo vya rushwa vinaendelea.

Kwa upande wake, Ofisa Uchunguzi Dawati la Elimu kwa Umma, Sabeth Mshana, alisema elimu ya rushwa inasaidia kwa kiasi kikubwa wananchi kujua haki zao za msingi katika maeneo mbalimbali wanayofanyia kazi.

Mshana alisema kampeni maalum iliyoanzishwa ina umuhimu mkubwa kwa wananchi, kwa kuwa inawafikia wananchi wengi na kwamba wameamua kwenda kwenye soko hilo kwa kuwa asilimia kubwa ni wanawake.

Mwenyekiti wa Soko la Bonanza, Marwa Mwita, alisema asilimia 98 ya wafanyabiashara wa samaki katika soko la Bonanza ni wanawake, hivyo taasisi hiyo imefanya vizuri kutoa elimu ya kuzuia rushwa katika eneo hilo.

# Elimu yatakiwa mradi wa uwekaji anwani za makazi

**Na Peter Mkwavila,**DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Dodoma, Jabir Shekimweri ameitaka Halmashauri ya Jiji la Dodoma kutoa mafunzo kwa vitendo kwa watu watakaotekeleza mradi wa uwekaji anwani za makazi ili kufanya kazi kwa ufanisi.

Shekimweri alitoa agizo hilo alipokuwa akizungumza na wakazi wa Kata ya Ipagala jijini hapa kwenye uzinduzi wa utekelezaji wa mfumo wa uwekaji wa anuani za makazi Dodoma.

Alisema ni muhimu pamoja na kuwapatia semina elekezi lakini wanapaswa kupatiwa mafunzo hayo ili kazi waifanye kwa uadilifu na uzalendo kwa taifa lao.

Shekimweri alisema uwekaji anwani hizo utafanyika kwenye mitaa 222 ya Kata 41 zilizopo jijini humo. Aidha, aliwataka kuhakikisha vijana watakaopata ajira hiyo ya muda ya utekelezaji wa uwekaji wa mfumo wa anwuani za makazi na postikodi miongoni mwao wawe wanaotoka maeneo wanayoishi.

"Mimi nitashangaa sana ikiwa halmashauri hii inaajiri vijana wa kutoka nje ya mikoa na kata na mitaa husika, litakuwa jambo la kuwahujumu vijana wetu hao, hivyo nitoe angalizo kuhakikisha watakaowaajiri wawe wanatoka maeneo wanaoishi na si vinginevyo," alisisitiza.

Hata hivyo, aliwataka vijana watakaopata ajira hiyo ya muda kuhakikisha wanaifanya kazi hiyo kwa uzalendo na uadilifu mkubwa ili kukamilisha kwa wakati.

Naye, Mratibu wa Mfumo huo kwa jiji hilo, Joseph Nkuba, alisema utekelezaji wa mradi huo mkubwa ni maelekezo ya Rais Samia Suluhu Hassan ya kutaka kabla ya sensa ya watu na makazi kufanyika zoezi hilo la uwekaji anuani liwe limefanyika.

"Halmashauri hii ya Jiji la Dodoma mradi ulianza rasmi Desemba 15 2021 kwa kutambua mipaka ya mitaa ya kiutawala ambapo mpaka sasa tumeitambua mipaka 153 kati ya mitaa 222 na mitaa 69 bado haijatambuliwa mipaka yake na zoezi linalofuatia ni kuitambua namba za nyumba na kuchukua taarifa za wakazi na kuzisajili kwa mfumo,"alisema.

# Wizara yataka kasi ujenzi jengo lake

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Elimu,Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, amemtaka mkandarasi kutoka kampuni ya CRJE anayejenga jengo la Wizara hiyo Mtumba jijini Dodoma, kuhakikisha anakamilisha kwa wakati na kuzingatia viwango vilivyopo kwenye mkataba wa ujenzi huo.

Akikagua ujenzi wa jengo hilo, Kipanga alisema ameridhishwa na kasi ya utekelezaji wa mradi huo na kwamba Wizara itahakikisha wanausimamia ili ukamilike kwa wakati.

"Nimpongeze sana mkandarasi kwa kuweka Programu ya kazi pamoja na vitendea kazi vipo vizuri unapofanya kazi kama hii ni lazima uwe na rasilimali watu, rasilimali fedha, vifaa, muda, menejimenti, ndio maana nilihitaji kuona hivi. Tunaamini tukisimamia vizuri kazi yetu itaenda vizuri," alisema.

Aliongeza: "Sisi Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tutahakikisha tunasimamia ujenzi huu kwa kushirikiana na wenzetu wa Chuo Kikuu cha Ardhi ambao ndio washauri wa mradi ili kazi hii iweze kukamilika."

Alisema mradi huo umeanza Desemba 15, 2021 na unatarajiwa kukamilika Desemba 15, mwaka huu ambapo zaidi ya Sh. bilioni 15 zinatarajiwa kutumika.

"Rais Samia Suluhu Hassan ameishazitoa fedha hizo kwa Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, haya sio kwenye Wizara ya Elimu tu yanajengwa katika Wizara na Taasisi zote,"alisema.

Mkadiriaji majenzi kutoka Chuo Kikuu cha Ardhi, Saudeni Anania, alisema awamu ya pili ya ujenzi huo inajumuisha ujenzi wa jengo la ofisi lenye jumla ya sakafu nane.

Alisema pia kuna kazi za nje ambazo ni ujenzi wa maegesho ya magari,bustani pamoja na fensi ambapo amedai jengo hilo linakadiriwa kuwa na jumla ya eneo la sakafu la mita za mraba 10,900.

Alibainisha mradi huo unaendelea vizuri ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia tano.

"Rai yetu kwa Wizara kwa pamoja tunaomba juhudi zaidi katika ufuatiliaji wa malipo ya mkandarasi pindi ambapo nyaraka zinapohusu malipo zinapowafikia kutoka kwa mshauri elekezi ili kuepusha ucheleweshwaji wa mradi,"alisema.





# Watoto wanaoishi mazingira magumu wapatiwa bima afya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

WATOTO 10 wanaoishi kwenye mazingira magumu katika Wilaya ya Mbeya wamenufaika na msaada wa kukatiwa bima za afya ili kuwasaidia kupata matibabu wanapougua pamoja na kupatiwa mahitaji mbalimbali ya nyumbani.

Msaada huo ulitolewa juzi na Exodus Women Group kinachoongozwa na Mtendaji wa Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mbalizi, Elizabeth Lyombe.

Alisema kikundi hicho kiliamua kuanza kutoa misaada hiyo kutokana na kubaini watoto wengi wanaoishi kwenye mazingira magumu wanapata matatizo ya kiafya na kushindwa kutibiwa na baadhi wanakosa mahitaji muhimu.

Alisema kikundi hicho kinawasaidia zaidi watoto ambao wanalelewa kwenye familia maskini tofauti na vikundi vingine ambavyo huwa vinawasaidia watoto wanaoishi kwenye vituo vya kulelea watoto yatima.

"Tulianza mwaka jana kwa kuanza na watoto watano ambao tuliwakatia bima za afya na leo tunawakabidhi watoto 10 bima pamoja na mahitaji muhimu, lakini tutaendelea kufanya hivyo ili kulisaidia kundi hili muhimu kwa taifa," alisema Lyombe.

Ofisa Ustawi wa Jamii wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Emiliana Mbise, alikishukuru kikundi hicho kwa msaada huo na kueleza wapo watoto wengi ambao wanaishi kwenye mazingira magumu.

Alivitaka vikundi vingine pamoja na watu wenye uwezo wa kiuchumi kuyasaidia makundi maalumu kwa maelezo kuwa misaada hiyo inasaidia kuzifariji familia hizo.

# TANROADS yapewa miezi 4 kuweka taa SIA

**Na Nebart Msokwa,** RUNGWE

SERIKALI imetoa miezi minne kwa Wakala wa Barabara nchini (TANROADS) kukamilisha ujenzi wa jengo la abiria pamoja na kuweka taa za kuongoza ndege katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Songwe (SIA).

Agizo hilo lilitolewa na Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Atupele Mwakibete, alipofanya ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa miundombinu ya uwanja huo na kutoridhishwa na kasi ya mkandarasi.

Alisema katika mradi huo alibaini kuwa uzio wa uwanja huo haujajengwa kwa viwango vinavyotakiwa na kuwataka kurudia kujenga katika maeneo ambayo yana upungufu.

Vilevile, alisema hakuridhishwa na kasi ya ujenzi wa jengo la abiria pamoja na uwekaji wa taa za kuongozea ndege na kuagiza kazi hizo zifanyike haraka na kukamilika kabla ya mwezi Julai.

"Kwenye taarifa zenu inaonyesha kwamba uzio mmeujenga kwa kuuzamisha mita moja, lakini taarifa nilizonazo ni kwamba mmedanganya, nina picha ambazo nilitumiwa kwenye simu zinaonyesha uzio unaning'inia," alisema Mwakibete.

Alisema kwa upande wa jengo lilitakiwa liwe limeshakamilika, lakini kila muda TANROADS ambao ndiyo waliopewa tenda ya kujenga jengo hilo bado hawajakamilisha na wameomba kuongezewa muda.

Hata hivyo, aliagiza TANROADS kuwasiliana na Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) ili wajenge barabara ya kuzunguka uwanja huo ili iwasaidie wananchi wa Kitongoji cha Iwejere ambao kwa sasa hawana mawasiliano ya barabara.

Alisema barabara hiyo itawasaidia zaidi wanafunzi wanaotoka katika kitongoji hicho ambao wanasoma katika Shule ya Msingi Ikumbi ambao kwa sasa wanazunguka umbali wa zaidi ya kilomita 10.

Awali, mwakilishi wa TANROADS, Mhandisi Abdallah Mziray, alisema wamechelewa kukamilisha mradi huo kutokana na vifaa vya ujenzi kuchelewa kufika kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa corona ambao ulisababisha baadhi ya nchi kufunga mipaka yake.

Alisema kwa sasa hawajapewa fedha za kutekeleza mradi huo na hivyo wanasubiri wakipata wataendelea kujenga na kwamba mpaka kufikia mwezi Julai watakuwa wamekamilisha.

Kwa upande wake Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, Dk. Rashid Chuachua, alisema kutokana na kusuasua kwa ujenzi wa miundombinu ya uwanja huo, anakusudia kupeleka vyombo vyake vya uchunguzi ili kubaini tatizo lililoko.

Dk. Chuachua alisema miundombinu ya uwanja huo ni muhimu ikamilike haraka kutokana na umuhimu kwa maendeleo ya Kanda ya Nyanda za Juu Kusini pamoja na nchi jirani za ukanda wa SADC.

Uwanja wa Ndege wa Songwe kwa muda mrefu ulikuwa umekwama kukamilika kutokana na matatizo mbalimbali, lakini hivi karibuni serikali ilitoa zaidi ya Sh. bilioni 18 kwa ajili ya kuukamilisha ikiwa ni pamoja na kuweka taa za kuongozea ndege ili zituwe saa 24.



Mkuu wa Wilaya ya Rungwe, Dk. Vincent Anney (wapili kulia), akikagua kitalu cha miche ya miparachichi iliyoandaliwa na moja ya vikundi vya wakulima wilayani humo, mkoani Mbeya hivi karibuni, kwa ajili ya kupanda msimu huu. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Wakulima wagaiwa miche 35,000 ya michikichi

**Na Nebart Msokwa,** KYELA

SERIKALI kupitia Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI) Kituo cha Uyole jijini Mbeya, imegawa miche 35,000 ya michikichi kwa wakulima wa zao hilo katika Wilaya ya Kyela ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kupunguza uagizaji wa mafuta nje ya nchi.

Miche hiyo ambayo iliandaliwa na TARI katika kitalu cha miche kilichoko Kyela Mjini, ilikabidhiwa kwa wakulima hao juzi na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, baada ya kufikia umri wa kupandwa.

Akizungumza wakati wa kukabidhi miche hiyo, Mtafiti wa michikichi kutoka TARI, Beatha Paul, alisema ikipandwa kitaalamu itatosha kwenye ekari 700 na kuongeza uzalishaji wa zao hilo katika wilaya hiyo.

Alisema miche hiyo ni ya kisasa na ina uwezo wa kuzaa mafuta tani nne mpaka tano kwa hekta moja tofauti na ya kienyeji ambayo wakulima wamekuwa wakiitumia siku zote ambayo inatoa tani moja kwa hekta moja.

"Michikichi hii inaanza kuzaa mapema kuliko ile ya kizamani, mkulima anaanza kupata matunda baada ya miaka mitatu pekee tofauti na ya kienyeji ambayo huwa inaanza kuzaa baada ya miaka mitano," alisema Beatha.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema michikichi ni miongoni mwa mazao yanayozalishwa kwa gharama ndogo zaidi na faida yake huwa ni kubwa kuliko mazao mengine ya mafuta ambayo yanazalishwa nchini.

Vilevile, Dk. Bucheyeki alisema mafuta yanayotokana na michikichi yana faida kiafya kuliko aina zingine za mafuta na kuwataka wakulima waliopatiwa miche hiyo kuzingatia hatua ambazo wanaelekezwa na wataalamu. Alisema miche hiyo ina uwezo wa kuvunwa kwa zaidi ya miaka 40 kuanzia inapopandwa na faida yake kwa wakulima ni kubwa huku akiwasisitiza kuachana na miche ya zamani.

"Tumefanya utafiti na kupima udongo ambapo tumebaini maeneo mengi yanafaa kwa kilimo cha michikichi na kakao katika wilaya hii, sasa tunawashauri wakulima waendelee kulima na kwa wanaoweza kumwagilia wanaweza wakawa wanavuna kila wiki," alisema Dk. Bucheyeki.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Godfrey Kingamkono, alisema miche waliyopewa wananchi bado haitoshelezi mahitaji ya wilaya hiyo na kuomba serikali kuongeza uzalishaji wa miche hiyo.

Alisema itakapoanza kuzaa itakuwa na faida kwa mwananchi mmoja mmoja na kuongeza mapato ya halmashauri kutokana na tozo mbalimbali. Akikabidhi miche hiyo kwa wananchi, Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Homera aliiagiza Halmashauri ya Kyela kuchukua asilimia tano ya mapato yanayotokana na michikichi kwa ajili ya uzalishaji wa miche mingine.

Aliitaka halmashauri hiyo kuwapatia TARI ili wao ndiyo wazalishe miche hiyo na uzalishaji ukiongezeka hata uagizaji wa mafuta nje ya nchi utapungua kwa kiasi kikubwa.



# Mil. 150/- zakusanywa faini makosa biashara

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAFANYABIASHARA 20 waliokiuka bei elekezi kwa bidhaa muhimu wamechukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria ikiwamo kufungiwa kwa muda na kulipa faini kwa makosa yao.

Waziri wa Biashara, Omar Said Shabani, aliyasema hayo jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Mfenesini, Machano Othman Said.

Machano alitaka kujua ni hatua gani zinazochukuliwa na serikali katika kukabiliana na tatizo la upandaji wa bei kwa bidhaa muhimu.

Waziri Shabani alisema jumla ya Sh. 15,100,000 zimelipwa na wafanyabiashara hao kama faini kwa waliokiuka bei elekezi.

Alisema Tume ya Ushindani ya Biashara kwa mujibu wa Sheria namba 5 ya mwaka 2018, kifungu cha 5 (c), umepewa jukumu la kusimamia na kupanga bei elekezi kwa bidhaa zilizodhibitiwa na serikali.

Alisema miongoni mwa hatua zilizochukuliwa na tume ni kufanya ukaguzi katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba kwa lengo la kuhakikisha bei elekezi inafuatwa kama zilivyotangazwa na serikali kupitia wizara yake.

"Mheshimiwa Spika, serikali mpaka sasa haijaweka mfumo wowote wa uagizaji wa bidhaa kwa wafanyabiashara. Serikali imetoa ruhusa kwa wafanyabiashara kufanya biashara kadiri ya uwezo wao lakini kwa kufuata taratibu zilizowekwa," alisema.

Alisema kwa mujibu wa Sheria Na. 5 ya Mwaka 2018, kutokuwapo ushindani halali wa biashara (monopoly) ni kosa chini ya kifungu cha 48 cha sheria hiyo.



Mwakilishi wa Jimbo la Mkokotoni, Haji Omar Kheri, akiuliza swali katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Zanzibar jana.
**PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# SMZ yaeleza matumizi fedha UVICO- 19

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imeweka bayana matumizi ya fedha za ahueni za ugonjwa wa UVIKO - 19 zilizotolewa na Serikali ya Tanzania Sh. bilioni 230 zitatumika kujenga shule, hospitali na barabara za ndani vijijini.

Akiwasilisha mchanganuo wa matumizi ya fedha hizo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi jana, Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Dk. Khalid Salum Mohamed, alisema tayari zimeanza kutumika kwa ujenzi wa hospitali 10 za wilaya za Unguja na Pemba zikiwa na hadhi ya kutoa huduma za wajawazito na watoto.

Waziri alisema serikali imeweka kipaumbele utekelezaji wa ujenzi wa hospitali hizo za vijijini ili kupunguza tatizo la wananchi kwenda mjini kutafuta huduma za afya na kusababisha usumbufu kwa kinamama na watoto.

Katika sekta ya afya, alisema serikali imetenga Sh. bilioni 68.5, kwa ajili ya ujenzi wa hospitali 10 za wilaya huku zikiwa na hadhi ya kutoa huduma za wajawazito na watoto.

Pia alisema Sh. bilioni 22 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali 11, huku Sh. bilioni 14 zikitengwa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali kubwa ya mkoa inayotarajiwa kujengwa Lumumba, Unguja.

Sh. bilioni 1.388, alisema zimetengwa kwa ajili ya kununua magari 11 ya kisasa ya kubeba wagonjwa huku Sh. milioni 500 zikiwa zimetengwa kwa ajili ya ununuzi wa mashine za kuchomea taka za hospitalini.

Katika sekta ya elimu, alisema serikali imetenga Sh. bilioni 68.5 kwa ujenzi wa shule za mjumuisho Unguja na Pemba pamoja na shule za ghorofa lengo likiwa kupunguza msongamano wa wanafunzi.

"Kwa mfano Sh. bilioni 16.45 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi wa madarasa 706 katika wilaya zote za Unguja na Pemba katika ngazi za maandalizi, msingi na sekondari," alisema.

Pia alisema serikali imetenga Sh. bilioni 6.25 kwa ajili ya ujenzi wa vyoo katika shule zikiwamo za msingi vipatavyo 1,693.

Alisema moja ya matatizo ambayo yamekuwa yakiwakabili wananchi wengi wa vijijini ni majisafi na salama ambapo wanawake na watoto ndio wanaopata usumbufu mkubwa asubuhi na mchana kutafuta huduma hiyo.

Katika kutatua tatizo hilo, alisema serikali imetenga ya Sh. bilioni 34.2 kwa ajili ya usambazaji wa huduma hiyo ambayo itahusisha moja kwa moja na kazi za kuchimba visima na kujenga minara ya matangi ya kuhifadhi maji.

Dk. Khalid alisema pia serikali imetenga Sh. bilioni 47.33 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi kazi za ujasiriamali kwa wananchi vijijini Unguja na Pemba.

Hata hivyo, alisema serikali inakusudia kufanya matengenezo makubwa barabara za ndani zinazokwenda vijijini jumla ya kilomita 230 na hivyo kupunguza tatizo kubwa la usafiri na kusaidia uzalishaji mali wa bidhaa mbalimbali.

## Madaktari bingwa India kuweka kambi Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, amesema madaktari bingwa kutoka India wanatarajia kuweka kambi Zanzibar kwa lengo la kuimarisha sekta ya afya nchini.

Aliyasema hayo jana ofisini kwake, Mnazi Mmoja wakati wa hafla fupi ya ujumbe kutoka India uliofuatana na Mkuu wa Biashara za Kimataifa, Somnath Shetty, kutoka Hospitali ya Wockhardt.

Mazrui alisema ujumbe huo unatarajia kushirikiana na Wizara ya Afya kwa kuimarisha huduma za afya kwa jamii pamoja na utoaji huduma za upasuaji kwa wagonjwa mbalimbali.

Aidha, alisema kesi ambazo mbalimbali wanatarajia kuzishughulikia zikiwamo kesi za wagonjwa wanaohitaji kusafirishwa nje ya nchi.

Alibainisha kuwa wanatarajia kushirikiana na serikali ya Zanzibar kupitia sekta ya afya kwa ajili ya kutoa huduma za matibabu bora kwa wananchi wake.

Waziri huyo alifurahishwa na ujumbe huo wenye lengo la kuisaidia Zanzibar katika utoaji wa huduma za afya na kueleza fursa hiyo itasaidia kuwajengea uwezo pamoja na ujuzi wa kiutendaji kupitia kwa madaktari bingwa kutoka India katika Hospitali za Mkoa na Wilaya.

"Serikali imejenga hospitali nyingi za wilaya na mikoa, hivyo ni fursa pekee ya kupata wataalamu hao ambao watasaidia kutoa ujuzi kwa wafanyakazi pamoja na kutoa huduma bora kwa wananchi," alisema Waziri Mazrui.

Naye Shetty alisema lengo la ujio wake ni kuleta ushirikiano wa pamoja katika kuwapatia huduma bora wananchi wa Zanzibar.

Alisema azma yao hiyo ni kuweka kambi ya madaktari bingwa Zanzibar kwa kutoa huduma za kiafya ikiwamo za upasuaji wagonjwa wenye kesi ambazo zinahitaji kusafirishwa nje ya nchi.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA**, NYUMBA INAUZWA KIJITONYAMA MAKUMBUSHO KARIBU NA KITUO CHA MABASI,WASILIANA NA **0654251570 AU 0686096001**

OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO MJINI ILIYOPO MOROGORO**

**TANGAZO KUITWA SHAURINI**

**SHAURI LA MADAI NAMBA: 279....2021**

**MDAI: DENIS METHEW**

**DHIDI YA**

**MDAIWA: ELI NASIFU CHUMA**

**Kwa: ELI NASIFU CHUMA**

**Ombi la mdai: DENIS METHEW**

**Madai ya : Pesa Shillings 489,143**

Unatakiwa kuhudhuria hapa Mahakamani katika shauri tajwa hapo juu bila kukosa.Shauri limepangwa kusikiliwa mnamo tarehe 23 mwezi 03 mwaka 2022 saa8:30 asubuhi.
Angalia kama hukuhudhuria/hamkuhuria siku iliyotajwa hapo juu.Mahakama itathibitisha kama umepokea/mmepokea kuitwa Shaurini,hii itaweza kutoa hukumu kuwa umeshindwa/mmeshindwa.
Hati hii yatolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 03 mwezi 03 mwaka 2022.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MACHA ALBERT TENDWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUZUKI CARRY yenye USAJILI NAMBA **T846 DKC,** CHASIS NAMBA: **DD51T530070, ENGINE NAMBA: F6A7663627.** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**KIL/MOS/RB/88493/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**WILIAM ADAM NGIMBA** ANATANGAZA kupotelewa na kadi ya GARI(LAND CRUISER) yenye namba za usajili **T 588 ANE**
Chassis namba: **LJ790007602**
Injini namba : **3380144**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi
taarifa ya polisi RB namba
**IRI/IRI/RB/81898/2022**

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya MAKOLE**

**Kituo cha MAKOLE MKOA DODOMA**

**Usimamizi wa mirathi Na 21/202**

**KATIKA SHAURI LA MIRATHI YA MAREHEMU FRANK REUBEN WA KISASA**

**KATIKA SHAURI LA MAOMBI YA KUMTEUA MSIMAMIZI YALIYOLETWA NA AGNES FRANK KALUMA**

**TANGAZO**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa Mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 28 Mwezi 03 Mwaka 2022 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
**Zingatia;**
Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Imetolewa leo tarehe 01 mwezi 03 mwaka 2022.

---

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**ANICETH LEKULES TEMBA**, Anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki Aina ya **Boxer,** yenye namba za usajili **MC 785 CJS** Yenye Chassis namba **MD2A21BY8KWF98570,** Engine namba **PFZWKF28231**
Yeyote atakayeona atoe taarifa kituo chochote cha polisi .
Polisi Taarifa :
**KIL/MOS/RB/28806/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABRAHAM A. IBRAHIM** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER** yenye usajili namba **T307 ACE, CHASIS NAMBA : gbj7509504000 ENGINE NAMBA:ipz0011275 .** kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
POLISI
**TAARIFA:ARU/ARU/82133/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**GODWIN COSMAS KAMONDO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **BAJAJI MKOMBOZI** yenye usajili namba **MC642ARN, CHASIS NAMBA : LYOHBMIC9EAF05640.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi
POLISI
**TAARIFA:GE/TR/RB/1047/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FEO GIRLS SECONDARY SCHOOL** inatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI FUSO** yenye **USAJILI NAMBA T970DBZ, CHASIS NAMBA: FP418FA20102.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**SO /RB/398/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ABDULSALAM MOHAMED** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **HYUNDAI EXCAVATOR** yenye USAJILI NAMBA **T649 BVJ, CHASIS NAMBA: LFNKGUKHIBAD22069.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**SO /RB/398/2022**

## KUPOTELEWA NA HATI YA KIWANJA

**RAMADHANI ATHUMANI HASSAN**
Anatangaza kupotelewa na HATI Yake ya Kiwanja Yenye **PLOT NO. 64 BLOCK "O"** MAPINDUZI NORTH Jijini Dodoma, Yeyote atakaeiona atoe tarifa Kituo chochote cha Polisi.
Taarifa ya Polisi
**DOD/DOD/RB/56620/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BIHONYI AUTO WORKS LTD** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA CROWN** yenye **USAJILI NAMBA T506 DEA, CHASIS NAMBA: GRS1835000204.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**SO /RB/398/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JESCA PASCAL MSIGWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **MITSUBISHI CANTER** yenye **USAJILI NAMBA T403 BJS, CHASIS NAMBA: FE638E530077.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
**POLISI TAARIFA:**
**SO /RB/398/2022**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EDWARD ANDREW** MASSUE anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya SUZUKI CARRY yenye usajili namba **T445 BQT.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
POLISI TAARIFA:
**DAR/OST/RB/81373/2022**

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe

*Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi*

*Kwa Bei Poa Tupigie 0782253676*

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

MASHAMBULIZI RUSSIA-UKRAINE:

# UN: Idadi ya wakimbizi kutoka Ukraine yavunja rekodi ya karne

● YAFIKIA MILIONI 1 NDANI YA SIKU TISA



Balozi wa Marekani katika Umoja wa Mataifa (UN), Linda Thomas-Greenfield akizungumza kwenye mkutano wa dharura wa 11 uliokutanisha wanachama wa umoja huo 193 kupiga kura kuhusu uvamizi wa Russia nchini Ukraine, makao makuu UN, Manhattan, jijini New York. Watu wanaokimbia mgogoro mjini Kyiv wakitarajia kuelekea mjini Lviv, nchini Ukraine kukimbia mashambulizi kwenye mji wa Kyiv, Ukraine, jana. **PICHA ZOTE:REUTERS**

**Kyiv,** UKRAINE

UMOJA wa Mataifa (UN), umesema idadi kubwa ya wakimbizi wanaokimbia nchini Ukraine, tangu Russia kuivamia nchi hiyo kwa takribani siku tisa leo, idadi ya wakimbizi imefikia milioni moja.

Miji mikubwa imeendelea kuzingirwa na kushambuliwa baada ya Kyiv, Kharkiv huku jana ikiwamo Mariupol pamoja na mji wa Kherson ambao una wakazi takribani 300,000.

Aidha mazungumzo ya amani yanatarajiwa kuendelea tena mara baada ya awamu mbili kumalizika bila kufikia mwafaka.

Mwendesha Mahakama ya Kimataifa ya Uhalifu wa Kivita (ICC), Karim Asad Ahmad Khan amesema timu ya mahakama hiyo ipo nchini Ukraine kwa ajili ya kuanza uchunguzi.

"Jana (juzi) niliunda timu kwa ajili ya kuelekea Ukraine, ," Khan alinukuliwa na shirika la habari la Reuters.

Amesema ofisi yake, itafanya utafiti kuhusu uhalifu utokanao na vita ikiwamo mauaji kwa pande zote mbili, Russia na Ukraine.

Wanajeshi wa Ukraine, wameendelea kuendeleza mashambulizi dhidi ya Russia, ingawaje mshauri wa Rais Ukraine Volodymyr Zelensky anasema:

"Tusaidieni kwa kuhakikisha kila dakika tunakabiliana na adui."

Inakadiriwa takribani wakazi wa Kyiv wa rika zote, watu wazima na watoto wapatao 150,000 wamejificha chini ya ardhi, huku jana usiku mji mkuu Kyiv, ukiendelea kulengwa.

Naibu Waziri Mkuu wa Ukraine, anasema Nato inahusika kwa kiasi fulani na vifo vya raia nchini humo kwa kushindwa kuweka zuio la ndege kuruka nchini mwake.

Akizungumza na BBC Radio 4, Olha Stefanishyna, anasema ni unyama kujua kwamba idadi ya raia na watoto watauawa kwa kutochukua uamuzi huo.

"Damu za hawa raia, ikiwa ni pamoja na mama na baba wa watoto wawili ambao walizaliwa jana tu na leo tu wanapoteza wazazi wao kwa kupigwa makombora, lawama sio tu kwenye mikono ya Russia."

Naibu Waziri Mkuu wa Ukraine, aliomba radhi kwa kutokuwa mwanadiplomasia katika chaguo lake la lugha, akisema alikuwa anazungumza akiwa ameketi kwenye makazi ya mabomu.

**MAZUNGUMZO YAENDELEA**

Wajumbe kutoka Russia na Ukraine jana walitarajiwa kukutana kwa mazungumzo nchini Belarus, ikiwa ni duru ya mazungumzo ya ana kwa ana tangu Russia ilipoivamia Ukraine siku tisa zilizopita.

Ripoti zinasema kuwa wawakilishi wa pande zote watakutana katika eneo la Brest nchini Belarus, linalopakana na Poland.

Katika hotuba ya video kwa taifa mapema jana, Rais Zelensky amewahimiza Waukraine kuendelea kupambana, lakini hakutaja kama Warussia, wamekamata miji yoyote.

Matamshi yake yamekuja wakati Russia ikikiri kwa mara ya kwanza tangu kuanza kwa uvamizi kuwa karibu askari 500 wameuawa katika mapigano na karibu 1,600 kujeruhiwa.

Idara ya Masuala ya Dharua ya Ukraine, imesema zaidi ya raia 2,000 wameuawa ijapokuwa ni vigumu kuthibitisha madai hayo.

Ofisi ya Haki za Binadamu imesema imerekodi visa vya raia 136 nchini Ukraine tangu Februari 24, mwaka huu.

**AFRIKA NA KURA DHIDI YA RUSSIA**

Wakati Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA), likiitisha upigaji kura kutoka nchi wanachama, kuhusu shutuma ya Russia kuivamia Ukraine, Eritrea pekee kutoka barani Afrika, imepiga kura kupinga uvamizi huo.

Kwenye kura hiyo mataifa 141 yaliunga mkono azimio hilo na kupingwa na mataifa matano na mengine 35 hayakuwamo kwenye mchakato wa kupiga kura.

Nchi 17 kutoka barani Afrika, ikiwamo Afrika Kusini, Algeria, Uganda, Burundi, Senegal, Sudan Kusini, Mali na Msumbiji hazijapiga kura kubainisha msimamo wowote.

Nchi zingine ni Sudan, Namibia, Angola, Zimbabwe, Equatorial Guinea, Jamhuri ya Afrika ya Kati (CAR), Madagascar, Tanzania na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC).

Uganda imesema inajiepusha na kura ya kuunga mkono kutokuwa upande wowote, ikiwa ni mwenyekiti anayekuja wa Vuguvugu la Nchi Zisizofungamana na Upande wowote (Nam).

Nam ni kongamano linaloundwa na nchi 120, zinazoendelea ili kudai uhuru wao kutoka kwa madai yanayoshindana ya mataifa hayo mawili makubwa.

Katika ujumbe wa Twitter, mwakilishi wa kudumu wa Uganda katika Umoja wa Mataifa (UN), Adonia Ayebare, amesema nchi hiyo itaendelea kujenga na kudumisha amani na usalama kikanda na kimataifa.

**KAULI YA UN**

Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa (UNGA), limepiga kura kwa wingi ya kuunga mkono azimio la kutaka Russia, kusimamisha mara moja mashambulizi nchini Ukraine na kuyaondoa majeshi yake yote nchini humo.

Mataifa mengi wanachama wa umoja huo yameonyesha kuliunga mkono azimio hilo. Kura hiyo iliyoitwa 'uvamizi dhidi ya Ukraine' ilipigwa katika kikao cha dharura cha baraza hilo.

Russia iliungwa mkono na Belarus, Syria, Korea Kaskazini na Eritrea, dalili inayoashiria namna taifa hilo lilivyotengwa kimataifa kufuatia uvamizi huo.

Katibu Mkuu UN, Antonio Guterres amewaambia waandishi wa habari baada ya kura hiyo kwamba, ujumbe wa UNGA uko wazi na ni dhahiri kwamba Russia inatakiwa kusimamisha mashambulizi Ukraine mara moja na kufungua milango ya mazungumzo na diplomasia.

Balozi wa Cuba ambayo haikuwamo kupiga kura, Pedro Luis Cuesta amelaumu kuhusu mzozo huo akisema umechochewa na matamanio ya Marekani ya kupanua jumuiya ya Nato.

***Imeandaliwa na Christina Mwakangale kwa msaada wa mtandao***

# BENKI YA ABSA ILIVYONOGESHA KILIMANJARO MARATHON 2022

**Na Mwandishi Wetu**

MBALI na wafanyakazi wake kushiriki kikamilifu, Benki ya Absa imeahidi kuendelea kutoa mchango wake katika mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon kwa kudhamini, imefahamika.

Akizungumza na gazeti hili mapema wiki hii, wakati wa maadhimisho ya 20 ya mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon, Mkuu wa Masoko na Uhusiano wa Benki ya Absa, Aron Luhanga, alisema tukio hilo ni jukwaa zuri kwa wafanyakazi wa benki hiyo kushirikiana na watu wengine sambamba na kutafuta soko zaidi kwa ajili ya bidhaa zinatolewa na taasisi hiyo ya kifedha.

"Lengo letu ni kuhakikisha wafanyakazi wetu wanaimarisha afya zao na ndiyo maana huwa tunawahimiza wawe washiriki katika tukio kama hili mara kwa mara," alisema na kuongeza Absa imekuwa ikiwafadhili wafanyakazi wake kushiriki matukio ya aina hiyo na kuhakikisha wanajiandaa vyema kabla ya ushiriki huo.

**Kuhusu mbio za Kilimanjaro Marathon ambayo hufanyika mjini Moshi kila mwaka na kushirikisha wanamichezo zaidi ya 12,000, Luhanga alisema wanajivunia kuwa sehemu ya mbio hizo muhimu kupitia ufadhili wao.**

Absa ni mmoja wa wadhamini waliopongezwa na aliyekuwa mgeni rasmi katika mbio za mwaka huu, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, ambapo aliisifu benki hiyo kwa mchango wake mkubwa kama moja ya wadhamini wa mashindano hayo.

Mbali na udhamini wake, banda la Benki ya Absa lililokuwa katika maonyesho yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi na kushirikisha wadhamini wengine, lilikuwa kivutio kwa washiriki na wageni wengine mbalimbali wa mbio hizo.

Aidha, wafanyakazi wa taasisi hiyo walioshiriki mbio hizo walionekana wenye furaha tele huku wakipiga picha na kufurahia nyakati hizo nzuri pamoja.

"Wafanyakazi wetu, wanafamilia na marafiki zao wamekuwa na wakati mzuri wakati uongozi wa benki ulipowakarisha hapa, wapo walioshiriki mbio hizo huku wengine wakiwa watazamaji," alisema na kuongeza wanajivunia kuwa sehemu ya maadhimisho ya miaka 20 ya Kilimanjaro Premium Lager Marathon.

Luhanga aliongeza mbali na ushiriki huo, Benki ya Absa pia ilikuwa mdhamini wa meza za maji kwa ajili ya washiriki wa mbio hizo zilizokuwa zimewekwa katika maeneo mbalimbali ya njia zilizotumiwa na wanariadha waliokuwa wanachuana.

Mbali na benki hiyo, wadhamini wengine wa mbio hizo ni Bia ya Kilimanjaro ambao ni wadhamini wakuu, Tigo (kilomita 21), Grand Malt (kilomita tano), huku wadhamini wa meza ya maji wakiwa ni Unilever Tanzania, TPC Sugar, Simba Cement, Maji ya Kilimanjaro, GardaWorld Security, Keys Hotel, Kibo Palace Hotel, Surveyed Plots Company Ltd, Bodi ya Utalii Tanzania na CMC Automobiles.

Mbio za Kilimanjaro Premium Lager Marathon zimeandaliwa na Kampuni ya Kilimanjaro Marathon na kuratibiwa hapa nchini na Executive Solutions.




Msanii wa Bongo Movie, Jacquiline Wolper, ambaye ni balozi wa bidhaa za EMINA akiwa ameshika bidhaa za Kampuni ya Bingwa Laboratories wakati wa utambulisho rasmi wa kuanza kupeperusha bendera ya kampuni hiyo yenye kampeni ya usafi katika shule na masoko mbalimbali nchini. Kulia ni Hussein Janowalla na Emmanuel Mwambete ambao ni wakurugenzi wa Kampuni ya Bingwa **PICHA: MIRAJI MSALA.**

# Bondia Dulla Mbabe azidi kujiimarisha

**Na Shufaa Lyimo.**

BONDIA wa ngumi za kulipwa hapa nchini, Abdallah Pazi 'Dulla Mbabe', amesema amejipanga vizuri kumkabili mpinzani wake, Amour Sheikh Haji katika pambano la fainali ya kumsaka bingwa wa Championi wa Kitaa litakalofanyika Machi 20, mwaka huu jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Pazi alisema lengo ni kuhakikisha anashinda na kuendeleza rekodi yake nzuri ya kushinda mapambano anayoshiriki.

"Nimefurahi kusaini mkataba wa pambano hilo, na sasa ninaendelea kujifua ili niuweke sawa mwili wangu kwa ajili ya kupata ushindi," alisema Dulla Mbabe.

Bondia huyo alisema pia pambano hilo linatarajiwa kuwa na ushindani kutokana na uwezo alionao mpinzani wake, lakini amewataka mashabiki wake waendelee kumwamini.

Aliongeza licha ya kukaa bila kuwa na pambano kwa muda mrefu, bado anaamini atafanya vizuri kutokana na kiwango chake kipo pale pale kufuatia mazoezi anayofanya kila siku.

## Mtibwa yarejesha matumaini Ligi Bara

**Na Saada Akida**

KOCHA Msaidizi wa Mtibwa Sugar, Awadhi Juma, amesema pointi nne walizopata katika michezo miwili waliyocheza hivi karibuni imeongeza morali ya wachezaji wake kuelekea michezo inayofuata ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mtibwa Sugar walianza kwa kupata ushindi wa mabao 2-1 dhidi ya Mbeya Kwanza na mchezo uliopita walitoka suluhu ya ugenini dhidi ya Tanzania Prisons.

Akizungumza na gazeti hili jana, Awadhi alisema matokeo hayo waliyopata yamesaidia kuongeza hali ya kujiamini kwa wachezaji wake na wataendelea kujituma zaidi katika michezo iliyopo mbele yao.

Kiungo huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar alisema ligi imekuwa na ushindani mkubwa na wapinzani wao wamekuwa imara huku akijipanga kwenda kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika michezo hiyo ili kutorudia makosa.

"Tumepata pointi nne jijini Mbeya, tunarejea nyumbani kujiandaa na michezo miwili tutakayocheza nyumbani, matarajio yetu makubwa ni kufanya vizuri kutokana morali na hali ya wachezaji wetu iliyoongezeka," alisema kocha huyo.

Aliongeza kuelekea katika duru la lala salama wamejipanga kuhakikisha wanafanya vizuri katika kila mechi iwe nyumbani au ugenini kwa ajili ya kujiweka katika nafasi nzuri kwenye msimamo wa ligi hiyo.

"Ushindani ulioko msimu huu ni mkubwa, kila timu inapambana kusaka matokeo mazuri, hakuna mechi ndogo na hatuna timu ndogo, mechi zote ni ngumu na ili kupata pointi ni lazima upambane," Awadhi alisema.

Mtibwa Sugar itawakaribisha Geita Gold FC utakaochezwa Machi 13, mwaka huu, wakati Aprili 3, mwaka huu itawavaa Kagera Sugar, mechi zote zikichezwa kwenye Uwanja wa Manungu, Turiani mkoani Morogoro.

Vinara wa Ligi Kuu Tanzania Bara ni Yanga wakati mabingwa watetezi ni Simba, zote za Dar es Salaam.

## ZISIKUPITE

### ANCELOTTI ANUKIA UNITED

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti mwenye umri wa miaka 62, ameibuka kuwa anayeongoza kuwania kiti cha kocha mpya wa Manchester United. (***Times - subscription required***)

### JAMES KURUDI EVERTON

KIUNGO wa Colombia aliyewahi kuichezea Everton, James Rodriguez mwenye umri wa miaka 30 amedokeza uwezekana wa kurejea kwenye klabu hiyo akitokea Qatar. (***Express***)

### MBAPPE MSHAHARA JUU

KLABU ya Paris Saint-Germain inajiandaa kumpa mkataba mpya mshambuliaji wake, Kylian Mbappe mwenye miaka 23 ambao utamfanya alipwe kiasi cha pauni 799,000 kwa wiki ili kusalia klabuni hapo, huku Real Madrid wakimwania pia mchezaji huyo wa kimataifa wa Ufaransa. (***Le Parisian, via Star***)

### SPENCE AGOMBEWA EPL

KLABU za Bayern Munich, Tottenham na Arsenal zinamwania mlinzi wa kulia wa Middlesbrough, Djed Spence mwenye umri wa miaka 21, ambaye kwa sasa anacheza kwa mkopo Nottingham Forest. (***Sky Sports***)

### SINGO AGEUKA LULU

TOTTENHAM Hotspur na Arsenal, pamoja na Liverpool, pia zinafikiria kupeleka dau kwa ajili ya kumnasa mlinzi wa kulia wa Torino, raia wa Ivory Coast, Wilfried Singo mwenye miaka 21, ambaye atapatikana kwa kitita cha pauni milioni 15. (***Football London***)

### BARCA KUIBOMOA CHELSEA

BARCELONA wana matumaini ya kumshawishi mlinzi wa Chelsea na Denmark, Andreas Christensen mwenye umri wa miaka 25, na mchezaji mwenzake, Cesar Azpilicueta (32), raia wa Hispania kujiunga na klabu hiyo kwa uhamisho huru mwishoni mwa msimu. (***Mundo Deportivo***)

### JOHNSON SOKONI RASMI

KOCHA wa Nottingham Forest, Steve Cooper amesema kiungo mshambuliaji wa Wales, Brennan Johnson mwenye miaka 20, atavurugwa na mazungumzo ya mkataba mpya au nia za kutakwa na klabu nyingine za Ligi Kuu England. (***Mirror***)

### MC GREGOR AITAKA CHELSEA

NYOTA wa ngumi na mieleka, Conor McGregor mwenye umri wa miaka 33, ameonyesha nia yake ya kutaka kuinunua Chelsea baada ya mmiliki wake, Roman Abramovich kusema ana mpango wa kuiuza klabu hiyo. (***Twitter***)

### LEWANDOWSKI NJIA PANDA

MSHAMBULIAJI wa Bayern Munich, Robert Lewandowski mwenye umri wa miaka 33 hajaamua bado kuhusu hatima yake, lakini amesema yuko tayari kwa uamuzi wowote. (***Sky Sports Germany, via 90min***)

### TCHOUAMENI ANUKIA BARCA

BARCELONA wanataka kumsajili kiungo wa Monaco, Aurelien Tchouameni mwenye umri wa miaka 22. (***Sport***)

### COSTA KUTUA BRAZIL

MSHAMBULIAJI wa zamani wa Hispania, Diego Costa mwenye umri wa miaka 33, anakaribia kutua Corinthians ya Brazil. (***Star***).

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# RUSSIA YACHANGIA CHELSEA KUNADIWA

**●●● Abramovich afunguka amefanya uamuzi mgumu lakini ni kwa faida ya klabu...**

**LONDON,** ENGLAND

MMILIKI wa Chelsea, Roman Abramovich amefanya uamuzi wa kuiuza klabu hiyo baada ya sakata la Russia kuishambulia Ukraine hali iliyotishia kutaifishwa kwa mali zake nchini England.

Katika ujumbe uliotumwa katika tovuti ya klabu hiyo, Abramovich ameweka wazi yamekuwa maamuzi magumu kwake, lakini amefanya hayo yote kwa ajili ya kulinda heshima ya klabu hiyo.

"Ningependa kushughulikia uvumi katika vyombo vya habari katika siku chache zilizopita kuhusiana na umiliki wangu wa Chelsea FC. Kama nilivyosema hapo awali, kila mara nimekuwa nikichukua uamuzi kwa nia njema ya klabu.

"Kwa hali ilivyo sasa, nimechukua uamuzi wa kuiuza klabu, kwani naamini hii ni kwa manufaa ya klabu, mashabiki, wafanyakazi, pamoja na wadhamini na washirika wa klabu.

"Uuzaji wa klabu hautaharakishwa bali utafuata taratibu zinazostahili. Sitaomba mkopo wowote ulipwe. Hii haijawahi kuwa biashara wala pesa kwangu, lakini kuhusu mapenzi safi kwa mchezo na klabu.

"Zaidi ya hayo, nimeiagiza timu yangu kuanzisha msingi wa hisani ambapo mapato yote kutokana na mauzo yatachangwa. Msingi huo utakuwa kwa manufaa ya waathiriwa wote wa vita nchini Ukraine. Hii ni pamoja na kutoa fedha muhimu kwa mahitaji ya dharura na ya haraka ya waathiriwa, pamoja na kusaidia kazi ya muda mrefu ya kurejesha amani.

"Tafadhali fahamu kuwa huu umekuwa uamuzi mgumu sana kufanya, na inaniuma sana kuachana na klabu kwa njia hii. Hata hivyo, ninaamini hii ni kwa manufaa ya klabu."

LIVE IN PLAY
CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 985

MECHI KALI
SIMBA
VERSUS
BIASHARA UNITED
1 | 1.30
X | 4.54
2 | 9.28

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# PSG YAPAMBANA KUMBAKIZA MBAPPE




**PARIS, Ufaransa**

MSHAMBULIAJI wa Paris Saint-Germain, Kylian Mbappe aliripotiwa kuhusishwa na kutimkia Real Madrid, lakini Mkurugenzi wa soka wa klabu hiyo, Leonardo amesema watafanya kila kitu kinachowezekana kumfanya nyota huyo kubakia.

Katika mahojiano ya kina na gazeti la L'Equipe, Leonardo alitoa ufafanuzi katika masuala yote.

Hakumwongelea Mbappe pekee, bali pia alizungumzia kuhusu Lionel Messi, usajili wa Sergio Ramos na mustakabali wa kocha, Mauricio Pochettino.

Leonardo alithibitisha bado hakuna ofa yoyote iliyotumwa kwa Mbappe, kufuatia ripoti za ofa ya mkataba wake wenye thamani ya euro milioni moja kwa wiki.

"Hatujapokea ofa maalum. Kuna kipengele muhimu: Nadhani kitu cha mwisho ambacho tutaweka katika mkataba huu ni fedha," alisema Leonardo.


"Tunataka kumweka katika mazingira bora zaidi ili kumfanya kuwa mchezaji bora zaidi.

"Hatujawahi kuzungumza juu ya fedha. Kwa sababu sio juu ya hilo. Mbappe ana thamani kubwa sana ambayo nadhani hiyo ni ya pili. Nadhani kuweka kiasi hicho, itachukua dakika mbili tu."

# Barca, Christensen wamalizana

**BARCELONA, Hispania**

KLABU ya Barcelona imekubaliana na mlinzi wa Chelsea, Andreas Christensen kwa ajili ya kujiunga nao mwisho wa msimu huku Mkurugenzi wa Michezo, Mateu Alemany akifunga safari kuelekea jijini London kukamilisha usajili huo.




Christensen amekuwa na Chelsea tangu mwaka 2012 baada ya kujiunga akitokea Brondby ya nchini Denmark, pia aliwahi kucheza kwa mkopo Borussia Monchengladbach inayoshiriki Ligi Kuu ya Ujerumani kabla ya kupata nafasi ya kucheza mara kwa mara Chelsea.

Christensen alikuwa ni moja ya wachezaji muhimu kwenye mafanikio ya kocha, Thomas Tuchel kwa miezi 13 na kumsaidia kuchukua ubingwa wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, UEFA Super Cup, pia alikuwepo kwenye mchezo wa nusu fainali ya Kombe la Carabao ambapo walishinda dhidi ya Tottenham Hotspur huku akikosa mchezo wa fainali dhidi ya Liverpool kwenye Uwanja wa Wembley.

Christensen ni moja ya mchezaji muhimu ambaye Chelsea wanamwacha aondoke bure kwenye majira ya joto, pia kuna Cesar Azpilicueta na Antonio Rudiger nao wapo kwenye mkumbo mmoja na pia wanaweza kuondoka bure.

Christensen ambaye amecheza michezo 54 ya kimataifa atahamia kwenye dimba la Nou Camp jijini Barcelona mwishoni mwa msimu

## HABARI MICHEZO

,669,400

# SIMBA BADO YAWAKOSA KIBU, MUGALU, DILUNGA

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI ikiendelea kukabiliwa na mechi ngumu za Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa, Simba imesema wachezaji wake watatu, Chris Mugalu, Denis Kibu na Hassan Dilunga bado ni majeruhi na hawajajua ni lini watarejea uwanjani, ingawa wote kwa sasa wameripoti kambini.

Meneja Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema wachezaji hao ambao hawakusafiri na timu kuelekea Niger na Morocco kucheza mechi za Kombe la Shirikisho Afrika, wameanza kufanyiwa vipimo na madaktari wa timu hiyo ili kujua maendeleo ya majeraha yao yalipofikia na baada ya hapo ndipo watawaambia wanaweza kurejea lini uwanjani.

"Wachezaji hao wamerejea kambini, wameendelea kupata matibabu siku zote hizi, na wataangaliwa na madaktari wetu ni wapi majereha yao yamefikia na ni lini watarejea kuitumikia Simba. Nadhani baada ya mechi dhidi ya Biashara United nina imani tutakuwa na majibu mazuri kuhusu maendeleo ya wachezaji wetu hawa watatu," alisema Ahmed.

Kwa sasa kikosi cha Simba kimeonekana kukumbwa na majeruhi wengi, mpaka sasa hata Thadeo Lwanga ambaye aliumia kwenye mechi ya marudiano ya Ligi ya Mabingwa Afrika katika mechi dhidi ya Jwaneng Galaxy ya Botswana iliyochezwa Oktoba 24, mwaka jana, pamoja na kuripotiwa amepona, lakini hadi sasa hajacheza mechi yoyote.

Kibu, aliumia katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Mbeya City iliyochezwa Januari 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa Sokoine Mbeya, Dilunga akiumia katika mazoezi ya timu hiyo wakati ikijiandaa na mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya Asec Mimosas kutoka Ivory Coast iliyochezwa Februari 13, mwaka huu huku Mugalu ambaye amekuwa na majeraha ya mara kwa mara, lakini mara ya mwisho alicheza mechi ya Kombe la FA na kufunga bao dhidi ya Dar City, Simba ikishinda mabao 6-0.

Simba ambao ni mabingwa watetezi leo wanatarajia kushuka dimbani kuwakaribisha Biashara United katika mechi ya raundi ya 16 itakayochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa Musoma, timu hizo zilitoka sare ya bila kufungana.

# Nani kushinda Sportpesa Jackpot?




Tarimba Abbas

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya burudani na michezo Sportpesa inapenda kuutaarifu, umma wa Watanzania, wadau na wapenda michezo ya kuwa Jackpot yao endelevu imefikia kiwango cha Sh. milioni 985.6.

Akizungumza na waandishi wa Habari jijini Dar es Salaam, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi, Tarimba Abbas alianza kwa kuwakaribisha wanahabari mkutano wa kampuni hiyo na kusema:

"Tunapenda kuchukua fursa hii kutoa taarifa kupitia vyombo vyote vya habari hapa nchini kwamba kwa sasa hakuna kampuni yoyote yenye dau kubwa zaidi ya hili na kumtangaza mshindi wa Jackpot kubwa kama hii, ambapo mpaka sasa hii ni mara ya tatu kwa Jackpot endelevu kupanda kwa dau zaidi ya nusu bilioni, baada ya kuanzia shilingi milioni 200.

"Kwa hakika, kiwango hiki kama hakitapata mshindi mwishoni mwa wiki hii, basi dau litakalofuata, litaweka historia ya kuwa dau la kwanza la ubashiri kufika bilioni moja kwa viwango vya Jackpot endelevu nchini.

''Tunapenda kuwasisitiza Watanzania wote kwa ujumla kucheza mara nyingi kadiri mwezavyo Ili kupata nafasi kubwa ya kushinda Jackpot hii nono ambayo ilianza kushindaniwa kuanzia mwezi wa 4, 2021 baada ya mshindi wa saba wa Jackpot Abdulaziz Ngámilo kupatikana.

"Jambo jema ama zuri kwa wachezaji ni kwamba hata kama hukufanikiwa kushinda dau hili moja kwa moja una nafasi nyingine ya kushinda kupitia Jackpot bonasi kwa washindi wanaopatia kuanzia timu 10,11 na 12," alisema Tarimba.

Tangu kuanza kwa Jackpot hii karibu miezi 11 Iliyopita, SportPesa tumeshatoa washindi wa kitanzania zaidi ya 200 kila wiki kwa waliobashiri kwa usahihi kuanzia mechi 10, 11 na 12.

"Washindi wa SportPesa Jackpot kwa mara ya kwanza walipatikana mwaka 2019 Agosti ambapo Magabe Marwa na Kingsley Pascal waligawana Sh. milioni 825.9 baada ya jackpot hii kukaa kwa miaka miwili."


## JACKPOT MECHI WIKI HII

### BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 05/03/22 | 18:00 | Wolverhampton vs Crystal Palace | 2.29 | 3.09 | 3.34 |
| 02. 05/03/22 | 18:00 | Newcastle vs Brighton | 2.70 | 3.14 | 2.70 |
| 03. 05/03/22 | 18:00 | Aston Villa vs Southampton | 2.30 | 3.36 | 3.06 |
| 04. 05/03/22 | 18:00 | Norwich City vs Brentford | 2.95 | 3.10 | 2.50 |
| 05. 05/03/22 | 20:00 | Roma vs Atalanta | 2.41 | 3.40 | 2.85 |
| 06. 06/03/22 | 14:30 | Genoa vs Empoli | 2.61 | 3.26 | 2.71 |
| 07. 06/03/22 | 16:00 | Cadiz CF vs Rayo Vallecano | 3.31 | 3.06 | 2.32 |
| 08. 06/03/22 | 17:00 | Reims vs Strasbourg | 3.48 | 2.78 | 2.39 |
| 09. 06/03/22 | 17:00 | Bordeaux vs Troyes | 2.29 | 3.48 | 2.93 |
| 10. 06/03/22 | 17:00 | Bologna vs Torino | 2.60 | 3.29 | 2.69 |
| 11. 06/03/22 | 19:00 | Antalyaspor vs Sivasspor | 2.57 | 3.21 | 2.67 |
| 12. 06/03/22 | 19:00 | Fenerbahce vs Trabzonspor | 2.38 | 3.21 | 2.91 |
| 13. 06/03/22 | 19:30 | FC Koln vs Hoffenheim | 2.70 | 3.40 | 2.50 |

## MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

### IJUMAA - 04/03/2022

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 16:00 | 2257 | Kagera Sugar vs Namungo | 2.36 | 2.60 | 3.42 |
| 18:30 | 1301 | Arab Contractors vs Pyramids | 4.64 | 3.45 | 1.76 |
| 18:30 | 5290 | Tsarsko Selo vs CSKA 1948 | 3.66 | 3.56 | 1.83 |
| 19:00 | 4389 | Simba vs Biashara United | 1.30 | 4.54 | 9.28 |
| 19:00 | 5829 | Ruzomberok vs Dunajska Streda | 2.27 | 3.14 | 2.94 |
| 20:00 | 1461 | Yeni Malatyaspor vs Adana Demirspor | 3.68 | 3.49 | 1.94 |
| 20:00 | 1594 | Midtjylland vs Viborg FF | 1.69 | 3.75 | 4.64 |
| 20:00 | 2770 | Doxa Katokopia vs Olympiakos Nicosia | 2.31 | 3.21 | 3.06 |
| 20:00 | 3238 | Lokomotiva Zagreb vs NK Osijek | 3.32 | 3.17 | 2.07 |
| 20:00 | 3795 | Stal Mielec vs Jagiellonia | 2.50 | 3.03 | 2.70 |
| 20:30 | 1880 | Hobro vs HB Koge | 2.29 | 3.22 | 2.83 |
| 20:30 | 5210 | Holstein Kiel vs Paderborn | 2.17 | 3.44 | 3.04 |
| 21:00 | 5550 | FC Helsingor vs Horsens | 2.03 | 3.42 | 3.18 |
| 21:30 | 1297 | Yverdon vs Sport FC-FC Wil | 1.95 | 3.56 | 3.27 |
| 21:30 | 2725 | Sepsi Osk vs U Craiova SA | 1.84 | 3.18 | 4.50 |
| 21:30 | 2883 | FC Stade LS Ouchy vs FC Winterthur | 2.17 | 3.28 | 2.99 |
| 21:30 | 5349 | Neuchatel Xamax vs FC Vaduz | 2.09 | 3.37 | 3.08 |
| 22:00 | 1242 | Roda Kerkrade vs Dordrecht | 1.22 | 6.10 | 9.84 |
| 22:00 | 1748 | Gyirmot FC vs MTK Budapest | 2.16 | 3.31 | 2.98 |
| 22:00 | 2020 | Vitesse Arnhem vs Sparta Rotterdam | 1.75 | 3.63 | 4.32 |
| 22:00 | 2335 | De Graafschap vs Jong AZ Alkmaar | 1.34 | 5.09 | 7.04 |
| 22:00 | 2631 | Copenhagen vs Randers | 1.66 | 3.69 | 4.92 |
| 22:00 | 2906 | MSK Deinze vs KVC Westerlo | 2.75 | 3.43 | 2.33 |
| 22:00 | 3149 | Telstar vs FC Oss | 2.28 | 3.27 | 2.93 |
| 22:00 | 3306 | Maastricht vs NAC Breda | 4.89 | 4.01 | 1.58 |
| 22:00 | 4326 | SBV Excelsior vs Den Bosch | 1.40 | 4.69 | 6.44 |
| 22:00 | 4386 | VVV Venlo vs FC Volendam | 3.37 | 3.57 | 1.97 |
| 22:00 | 5907 | Helmond Sport vs FC Eindhoven | 3.91 | 3.66 | 1.80 |
| 22:15 | 1401 | FC Aarau vs FC Schaffhausen | 1.58 | 4.05 | 4.53 |
| 22:30 | 5375 | Pogon Szczecin vs Radomiak Radom | 1.65 | 3.48 | 4.83 |
| 22:30 | 5467 | Arminia Bielefeld vs Augsburg | 2.45 | 3.17 | 2.93 |
| 22:45 | 1457 | Cobh Ramblers vs Treaty United | 3.23 | 3.28 | 2.06 |
| 22:45 | 1673 | Wexford Youths vs Athlone Town | 2.12 | 3.61 | 2.84 |
| 22:45 | 2276 | Inter vs Salernitana | 1.16 | 7.43 | 15.06 |
| 22:45 | 2881 | St Truiden vs Mechelen | 2.28 | 3.35 | 2.95 |
| 22:45 | 3000 | Flint Town United vs The New Saints | 5.01 | 4.43 | 1.48 |
| 22:45 | 3081 | Drogheda Utd vs UCD Dublin | 1.88 | 3.28 | 3.81 |
| 22:45 | 3537 | Newtown AFC vs Bala Town | 2.07 | 3.67 | 2.90 |
| 22:45 | 3913 | St Patricks vs Shamrock Rovers | 3.42 | 3.18 | 2.03 |
| 22:45 | 4160 | Cliftonville Belfast vs Coleraine FC | 1.80 | 3.37 | 4.04 |
| 22:45 | 4430 | Shelbourne vs Derry City | 3.19 | 3.09 | 2.16 |
| 22:45 | 4910 | Huddersfield vs Peterborough | 1.55 | 3.93 | 5.50 |
| 22:45 | 5625 | Partick Thisle vs Inverness | 2.40 | 3.18 | 2.84 |
| 22:45 | 5695 | Cefn Druids vs Aberystwyth Town | 6.55 | 5.01 | 1.34 |
| 22:45 | 5962 | Sheffield Utd vs Nottingham | 1.97 | 3.33 | 3.67 |
| 23:00 | 4066 | Finn Harps vs Bohemians FC | 3.33 | 3.19 | 2.06 |
| 23:00 | 4117 | Lorient vs Lyon | 4.27 | 3.73 | 1.78 |
| 23:00 | 4520 | Zaragoza vs Almeria | 3.29 | 3.04 | 2.24 |
| 23:00 | 4909 | Alaves vs Sevilla FC | 4.30 | 3.30 | 1.91 |
| 23:15 | 4844 | Gil Vicente vs GD Estoril | 1.95 | 3.36 | 3.80 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Ijumaa Machi 4, 2022

Nipashe



## Russia yachangia Chelsea kunadiwa

NAMBA MOJA



Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla (kulia), akionyesha kadi yake ya kidijitali ya Yanga baada ya kukabidhiwa katika hafla fupi iliyofanyika Zanzibar jana. Kushoto ni Mjumbe wa Kamati ya Mabadiliko ya klabu hiyo, Hersi Said. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, BIASHARA KUMALIZA UBISHI

●●●Ingawa Pablo alalamika hali ya uchovu, majeruhi ni tatizo...

**Na Saada Akida**

HAKUNA kupoteza. Hii ni kauli ya mabingwa watetezi, Simba ambao wanatarajia kuwakaribisha Biashara United kutoka Musoma katika mchezo wa raundi ya 16 wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam.

Simba imeweka wazi licha ya kuwa nyuma kwa idadi ya pointi dhidi ya vinara Yanga, bado lengo lao ni kuhakikisha wanatetea ubingwa wao.

Wekundu wa Msimbazi wamedhamiria kuhakikisha wanashinda mechi zote 15 za mzunguko wa pili ili kutimiza malengo yao ya kulibakisha taji ndani ya klabu yao.

Akizungumza jijini jana katika makao makuu ya Shirikisho la Soka Tanzania, (TFF), Kocha Mkuu wa Simba, Pablo Franco, alisema mechi ya leo itakuwa ngumu kwa sababu ya wao kutopata muda wa kupumzika ingawa ana imani vijana wake wataingia dimbani kusaka pointi muhimu katika mchezo huo.

Pablo alisema itakuwa ni mechi yenye ushindani na wao wamejiandaa kupambana kuhakikisha wanapata matokeo mazuri na kupunguza tofauti ya idadi ya pointi dhidi ya vinara ambao ni watani zao, Yanga.

"Tumejipanga vizuri kuhakikisha tunapata pointi muhimu na kikosi changu kipo tayari kuwavaa Biashara United katika mchezo huo," alisema Pablo.

Kocha huyo alisema kila mechi kwao ni muhimu na kwao hakuna mechi rahisi kwa sababu wanatakiwa kutopoteza pointi hata moja.

Aliwataja wachezaji watakaokosa mechi ya leo ni pamoja na Aishi Manula, Mzamiru Yassin, Sadio Kanoute, Rarry Bwalya, Denis Kibu, Chris Mugalu na Tadeo Lwanga.

Naye Kocha Mkuu wa Biashara United, Vivier Bahati, alisema mechi hiyo itakuwa nzuri na maandalizi waliyofanya yaliendana na aina ya mpinzani wanaekutana naye.

Vivier alisema wachezaji wote 24 walikuja jijini wako fiti na hakuna majeruhi na matarajio yake makubwa ni kuondoka na matokeo chanya.

"Tunajua ubora wa Simba, tunaheshimu kiwango cha Simba, wanatoka kimataifa wamefanya vizuri mechi moja na kupoteza, tutaingia kwa tahadhari kubwa kuhakikisha tunafikia malengo yetu katika mchezo huu," alisema Vivier.

Aliongeza wataingia kwa kujilinda na wakipata mpira watacheza kwa kushambulia ili kuhakikisha wanapata kile ambacho wamekuja kukitafuta walipotoka Mara.

Nahodha wa Biashara United, Abdulmajid Mangalo alisema timu yao imejiandaa vizuri kuhakikisha wanapata matokeo mazuri.

"Tumejipanga vizuri, kocha wetu (Vivier), amefanya kazi yake kubwa, imebaki kwetu kuhakikisha tunapambana kutafuta pointi muhimu katika mchezo huo," alisema Mangalo.

Simba itashuka uwanjani leo ikiwa na kumbukumbu ya kulazimishwa sare ya bila kufungana na Biashara United, katika mchezo wao wa kwanza wa fungua dimba uliochezwa kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mwaka jana.

## Kiwango Geita chaitisha Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze amesema wanakwenda kuikabili Geita Gold kwa tahadhari kubwa kwa sababu tayari wamepata taarifa zote kuhusu kuimarika kwa wapinzani wao ambao wanashiriki Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu kwa mara ya kwanza.

Kaze, raia wa Burundi alisema mechi hiyo itakuwa ngumu kutokana na kucheza ugenini, lakini wapinzani wao wamekuwa na rekodi nzuri katika mechi zao za nyumbani.

Kocha huyo alisema wanafahamu Geita Gold ni moja ya timu nzuri zinazoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara huku ikiwa pia na baadhi ya wachezaji wenye uzoefu, hivyo watalazimika kuongeza umakini katika mchezo huo ili wapate matokeo mazuri.

"Maandalizi yanakwenda vizuri sana, mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu Geita Gold inafanya vizuri katika mechi zake mfululizo, wamepata matokeo mazuri kwenye mechi zao nne au tano zilizopita. Wameimarika, wamejijenga na kupata wachezaji wazuri katika kipindi cha dirisha dogo, kwa hiyo tunajua hilo, lakini lengo letu ni pointi tatu, tutakwenda kwa tahadhari," alisema kocha huyo.

Naye kiungo, Feisal Salum 'Fei Toto', alisema haitokuwa mechi rahisi, lakini yeye na wachezaji wenzake, wanaahidi kupambana ili kupata ushindi.

"Mechi itakuwa ngumu, lakini sisi kama wachezaji tutapambana na kuwapa ushindi, kikubwa tuombe Mungu tu," alisema Fei Toto.

Farid Mussa, ambaye hivi karibuni aliimudu vyema nafasi ya beki wa kushoto wakati kiasili ni winga wa kushoto, alisema kwa sasa makocha wao wanarekebisha mapungufu yaliyojitokeza katika mechi dhidi ya Kagera Sugar ili mchezo unaofuata wafanye vizuri zaidi.

"Tumecheza vizuri, lakini pamoja na mazuri kulikuwa na mapungufu ambayo kwa sasa yanafanyiwa kazi ili Jumapili tupate ushindi," alisema Farid ambaye anacheza beki ili kuziba pengo la Kibwana Shomari ambaye ni majeruhi.

Ofisa Habari wa Yanga, Hassan Bumbuli, alisema kikosi cha timu hiyo kitaondoka leo kuelekea Mwanza kwa ajili ya mchezo huo wa Ligi Kuu Tanzania Bara raundi ya 17 utakaochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa CCM Kirumba jijini humo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >